

**SAKA MAJANGA ARSENAL**

UKURASA 22

**VIDEO** ya mwanamke yawaponza wapigaji makachu Forodhani

UKURASA 2

**MWINYI** azindua miradi mitano ya kuongeza ufanisi viwanja vya ndege

UKURASA 3

**KASI** kesi ubakaji, ulawiti yawaibua majaji wanawake

UKURASA 4

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe


Jumatatu Desemba 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581899
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digi edigital

# Mbowe ashtukia jambo CHADEMA



## ARUDISHA fomu akiwa na angalizo kwa Lissu, wanachama... *Ukurasa wa 2*



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Blasius Chatanda (wa pili kushoto) akimweleza jambo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa walipofika juzi usiku katika Kijiji cha Nyabukome wilayani Biharamulo mkoani Kagera ilikotokea ajali ya basi na kusababisha vifo vya watu 11 na kujeruhi 16. **PICHA: RESTUTA DAMIAN**

## Ajali ya basi ilivyoua watu 11, kujeruhi 16

UKURASA 2

UKURASA WA 7

## ASHIKILIWA KWA TUHUMA KUMUUA MZAZI MWENZAKE, KUTUPA MWILI BARABARA KUU

JESHI la Polisi mkoani Arusha linamshikilia mkazi wa Makumira wilayani Arumeru, John Maganga (26) kwa tuhuma za mauaji ya Safina Emanuel (19), mama lishe na mkazi wa Magadirisho wilayani humo.
Akitoa taarifa hiyo jana, Kamanda wa...

UKURASA WA 23

## FADLU AFURAHIA 5G AKIKERWA SIMBA KURUHUSU MABAO

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu David, ameonesha furaha kwa timu yake kupata ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Kagera Sugar, akisema ni mkubwa...

## Mganga kienyeji akamatwa ndani ya basi akidaiwa kusafirisha zana zake kwa kutumia utumbo wa samaki

UKURASA 3

**MICHEZO** OLD TRAFFORD MPYA KUJENGWA ZANZIBAR UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Mbowe ashtukia jambo CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe amerejesha fomu ya kugombea tena nafasi ya uenyekiti wa chama hicho huku akitoa angalizo kwa wanachama na wafuasi wa chama hicho kutotumia uchaguzi huo kuharibu taswira ya chama.

Ameagiza mamlaka za chama zinazohusika kusimamia uchaguzi huo, zihakikishe unakuwa huru na wazi ili usiwe na doa. Atakayeshinda awe na uhalali mbele ya wanachama wa chama hicho.

"Ninaagiza mamlaka za chama zinazohusika na kusimamia mkakati wote ama mchakato wote wa uchaguzi pamoja na uchaguzi wenyewe, zihakikishe uchaguzi wetu unakuwa safi usiokuwa na doa, uwe wazi, kila mtu aone, dunia ione kwamba CHADEMA tunaweza kuchaguana bila kufanya wizi wa kura kwa sababu wizi si asili yetu," alisema Mbowe baada ya kurudisha fomu katika ofisi za chama hicho Dar es Salaam jana.

Mbowe aliongeza: "Yeyote atakayepatikana akawe na uhalali mbele macho ya wanaCHADEMA, mbele ya macho ya dunia na zaidi mbele ya macho ya Mungu. Ninawaombea sana wale ambao watashindana katika kampeni, ninarudia mara kwa mara, kafanyeni kampeni za kujenga taasisi yetu na msijenge kampeni za kuumizana kwa mambo ambayo si ya kweli.

"Tukawe watu wa kweli wa kukilinda chama chetu, viongozi, kulinda wagombea na wanachama wetu. Sisi ni familia, u-familia wetu hauwezi ukafa kwa sababu ya uchaguzi."

Mbowe alisema anatamani ijengwe CHADEMA yenye ustahimilivu, yenye viongozi wanaoweza kukutana na changamoto lakini wakawa wastahimilivu.

"Tunatamani tukaijege CHADEMA yenye viongozi wabunifu, tukafanye mabadiliko yote tunayofikiri yakifanywa yatakifanya chama chetu kuwa bora zaidi katika malengo yetu ya kupigania haki ya watu wake, uhuru wa watu wake, demokrasia ya watu wake na hatimaye maendeleo ya watanzania wote katika ujumla wake," alisema.

Mbowe alitoa tahadhari kuwa wapo baadhi ya viongozi ambao tayari wameshaanza kutoka nje ya mstari kwenye kampeni zao kuelekea uchaguzi huo na kwamba wanawaombea ili wafanye kampeni za kistaarabu na si za kupasua chama au kuumizana.

"Tunatambua kuna wengine ambao wanatoka nje ya mstari katika kutengeneza kampeni chafu za matusi, hiyo si tamaduni wala si tabia ya CHADEMA, tunawaomba wale wote waliopendekeza kampeni za kutugawa, basi wakapate busara ya kuachana na kampeni za kutugawa.

Uchaguzi wa chama hicho unatarajiwa kufanyika Januari mwakani. Nafasi zinazogombaniwa ni pamoja na ya Mwenyekiti wa Chama Taifa, Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar. Nyingine ni Katibu Mkuu Baraza la Wazee (BAZECHA) Bara, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Mwekahazina.

Pia zipo za wajumbe watano wa Baraza Kuu ambao wanne kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Tanzania Zanzibar pamoja na wajumbe 20 wa mkutano mkuu ambao 15 ni wa kutoka Tanzania Bara na watano ni kutoka Tanzania Zanzibar.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi mkoa wa Iringa Daud Yassin (kushoto) akimkabidhi tuzo ya shukrani mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Salim Abri Asas kwa kukisaidia chama hicho. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Ajali ya basi ilivyoua watu 11, kujeruhi 16

**Na Vitus Audax**

WATU 11 wamefariki dunia huku wengine 16 wakijeruhiwa katika ajali ya basi la abiria Kampuni ya Capco One lenye namba za usajili T857 DHW lililofeli breki katika mteremko na kurudi nyuma kisha kupinduka.

Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Brasius Chatanda alisema ajali hiyo ilitokea juzi Desemba 21 saa nane mchana katika Kijiji cha Kabukome, kata ya Nyarubungo, wilayani Biharamulo kwenye eneo la mlima wa kuanzia pori la Kasindaga wakati gari hilo likitoka mkoani Kigoma kuelekea Bukoba, mkoani Kagera.

Kamanda Chatanda alisema chanzo cha ajali hiyo ni mfumo wa breki wa gari hilo kufeli wakati dereva alipolazimisha kusimama katika mlima ili kuruhusu kondakta wa gari hilo kumshusha mtoto ambaye alikuwa amepitilizwa kituo na kumfaulisha katika gari lingine lililokuwa likirudi uelekeo wa kituo alichotakiwa kushuka mtoto huyo.

"Gari lilipotoka Biharamulo kwenda Bukoba lilimpitiliza mtoto mmoja kituo cha kushuka, wazazi wakapiga simu kuwajulisha, hivyo dereva alipokutana na gari aina ya Coaster katika mlima ule, kwa sababu ya haraka akasimamisha gari mlimani na kondakta akashuka na mtoto amwahishe kwenye gari hilo.

"Isivyo bahati, mfumo wa gari upande wa breki na gia vyote vikagoma, gari likaanza kurudi nyuma, likamshinda dereva, likatoka nje ya barabara na kubinuka na kusababisha vifo na majeruhi.

Miili yote ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Biharamulo huku watu 16 wakijeruhiwa na baadhi yao wanaendelea vizuri hospitalini hapo," alisema Kamanda Chatanda.

Akithibitisha kupokea miili na majeruhi hao, Mganga Mkuu wa Hospitali Teule ya Biharamulo, Gresmus Sebuyoya alisema walipokea miili ya watu 11. Kati yao, wanaume ni wanne, wanawake watano, mtoto wa kiume mmoja na wa kike mmoja na kuwa miili yote imehifadhiwa hospitalini huko.

Kuhusu majeruhi, alisema 26 tayari wameruhusu huku wengine 16 wakiendelea na matibabu na uangalizi wa karibu.

Dk. Gresmus alisema waliobaki hospitalini huko kwa uangalizi na matibabu ni pamoja na watoto wanne ambao wanaendelea vizuri, wanaume sita pamoja na wanawake sita.

Akizungumza baada ya kutembelea majeruhi hospitalini, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa, alisema wizara imeanza kufanyia kazi maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufanya marekebisho ya kuwa na mfumo wa leseni.

Alisema katika mfumo huo wa leseni za udereva, utakuwa ukiwapunguzia alama madereva wanaofanya makosa yenye kuhatarisha usalama barabarani ambazo zitasaidia kuwafungia leseni.

Alitoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wote walioguswa na ajali hiyo na kutoa wito kwa watanzania kuendelea kuwaombea majeruhi wapone haraka.

"Nitumie nafasi hii kuombea roho za marehemu ambao tumewapoteza katika ajali ambayo imetokea hapa Biharamulo, tumepoteza ndugu zetu 11, wametangulia mbele za haki," alisema Waziri Bashungwa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Video ya mwanamke yawaponza wapigaji makachu wa Forodhani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar imetangaza kusimamisha shughuli za upigaji mbizi baharini, maarufu makachu, katika eneo la Forodhani.

Mamlaka hiyo imetoa taarifa hiyo kufuatia matukio ya ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo yaliyojitokeza kwa vijana wa makachu katika eneo la bustani ya Forodhani na kuleta athari mbaya kwa jamii na miundombinu ya serikali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka hiyo jana kupitia kitengo cha habari na uhusiano, matukio hayo yanajumuisha upigaji makachu kwa kutumia mavazi yanayokwenda kinyume cha utamaduni, uharibifu mkubwa wa mifereji na miundombinu mengine.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa kufuatia matukio hayo, mamlaka imesimamisha shughuli hizo za makachu hadi hapo itakapokamilisha kuandaa utaratibu wa kuimarisha usimamizi wa shughuli hizo.

Mamlaka hiyo inasema katika taarifa yake hiyo kuwa serikali inatambua mchango wa makachu kutangaza utalii na mamlaka hiyo inaendelea na uchunguzi wa jambo la ukiukwaji maadili na wahusika watakapobainika watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Hivi karibu katika mitandao ya kijamii kulisambazwa video ikimwonesha mwanamke akiruka makachu katika eneo la Forodhani akiwa na nguo za ndani tu huku maumbile yake yakiwa yanaonekana, jambo ambalo liliibua taharuki kwa wananchi, wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu.

"Mamlaka kwa kushirikiana na wadau na watumiaji wa Mji Mkongwe inaziomba taasisi za umma na binafsi pamoja na wananchi wote kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za watu wanaofanya vitendo kama hivyo ili wachukuliwe hatua.

"Kwa pamoja tunaweza kulinda na kuendeleza mji huo ambao ni urithi wetu wa kihistoria na kiutamaduni," mamlaka hiyo inaeleza katika taarifa yake hiyo.

Kabla ya kutolewa taarifa hiyo, Balozi Mdogo wa Brazil, Abdulbasit Abdulsamad, alilaani tukio hilo ambalo alisisitiza halileti taswira nzuri kwa Zanzibar na linakwenda kinyume cha maadili ya wazanzibari.

Shughuli za upigaji makachu katika eneo hilo la Forodhani zimeijengea umaarufu mkubwa Zanzibar katika mataifa mbalimbali duniani na kuitangaza kiutalii. Wageni wengi huminika katika eneo hilo kujionea na wengine kushiriki shughuli hiyo ambayo imeongeza ajira kwa vijana.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

# Akamatwa ndani ya basi akidaiwa kusafirisha vifaa vya uganga kienyeji

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MGANGA wa kienyeji, Juma Lugendo (30), mkazi wa Kahama, mkoani Shinyanga, amekamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida akidaiwa kusafirisha vifaa vya uganga na dawa za kienyeji zilizochanganywa na utumbo mbichi wa samaki ndani ya basi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Desemba 19 mwaka huu saa 12:30 jioni, maeneo ya mlima Sekenke, kata ya Ulemo wilayani Iramba, mkoani Singida.

Alisema mtu huyo alikuwa anasafirisha vitu hivyo ndani ya basi la kampuni ya Frester lenye namba za usajili T 794 EHR lililokuwa linatoka Kahama kwenda Dar es Salaam.

Kamanda Kakwale alisema polisi waliokuwa doria katika barabara ya Singida-Nzega, walipata taarifa zilizoenezwa kupitia mitandao ya kijamii kwamba ndani ya basi hilo mlikuwa na mtu aliyekuwa anasafirisha kichwa cha mtoto ambacho kilikuwa kinatoa harufu mbaya na kusababisha kero kwa abiria wengine.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, polisi waliweka mtego na kumkamata mtuhumiwa huyo na kumpeleka katika kituo kidogo cha polisi cha Misigiri ambako baada ya upekuzi, alikutwa na vifaa vinavyotumika katika uganga wa kienyeji na dawa za kienyeji ambazo zimechanganywa na utumbo mbichi wa samaki.

Kamanda Kakwale alisema mtuhumiwa baada ya kukamatwa, alifikishwa mahakamani akikabiliwa na kosa la kufanya shughuli za uganga wa kienyeji bila kuwa na kibali.

"Jeshi la Polisi linatoa onyo kali kwa wananchi wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii kwa kutoa taarifa za uongo na kusababisha taharuki kwa jamii," ilieleza taarifa hiyo ya Kamanda Kakwale.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Paul Walalaze, Meneja wa Elimu kwa walipakodi kutoka TRA (wanne kushoto) akikabidhi keki kwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo aliyepokea kwa niaba ya Naibu Meneja Mkuu wa kampuni ya The Guardian Ltd, Jackson Paul (watano kushoto) ikiwa ni shukrani kwa kampuni hiyo kuwa mmoja wa walipa kodi wazuri katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Dk. Mwinyi azindua miradi mitano ya kuongeza ufanisi viwanja vya ndege

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema, uimarishaji miundombinu katika viwanja vya ndege, unalenga kuvifanya kuwa bora na kutoa huduma kulingana na vigezo vya kimataifa.

Alitoa kauli mwishoni mwa wiki alipozindua miradi mitano ya miundombinu mbalimbali katika Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, wilaya ya Magharibi B, ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema lengo ni kuwa na viwanja vya ndege vyenye sifa ya utoaji huduma bora kwa abiria zitazokidhi mahitaji ya ongezeko la wageni wanaoingia nchini kila siku.

Alisema miradi mitano aliyozindua itafanya uwanja huo kuwa wa kujivunia na hadhi ya kimataifa katika Afrika na duniani kwa utoaji huduma bora zitakazoridhiwa na wageni.

Miradi aliyozindua Dk. Mwinyi ni pamoja uwekaji mawe ya msingi kwa majengo ya abiria 'Termninal One' na 'Two', ambayo alisema itajumuisha ujenzi wa jengo la viongozi na wageni mashuhuri (VIP) utakaotumiwa pia na wafanyabiashara wakubwa kupokea ndege binafsi za wageni mashuhuri.

Akizungumzia ujenzi wa kituo cha kisasa cha biashara, Rais Dk. Mwinyi alisema utahusisha majengo ya benki, migahawa mikubwa ya kimataifa na ofisi zitakazotoa huduma saa 24 kwa wageni na watumiaji wa uwanja huo pamoja na uzinduzi wa taa mpya za kuongozea ndege na mradi wa kituo cha mafuta ya ndege.

Rais Dk. Mwinyi alisema kituo hicho cha mafuta kitaleta ushindani katika utoaji huduma za mafuta kwa ndege zinazotua uwanjani huko na kutoa unafuu wa bei na kupunguza safari za ndege kwenda kuweka mafuta nje ya Zanzibar.

Akizungumzia Uwanja wa Ndege wa Pemba, Rais Mwinyi alisema serikali imekusudia kujenga kuwa wa kimataifa kwa kuutanua na kuongeza njia za kuruka na kutua ndege ili kuifungua Pemba kibiashara.

Alisema Pemba ijayo itapokea wageni na watalii moja kwa moja badala ya kushuka Zanzibar na hatimaye kuunganisha ndege nyingine kwenda Pemba. Alisema mradi huo unatekelezawa sambamba na ujenzi wa bandari za Mkoani, Wete na Shumba Mjini ili kuikuza Pemba kwa utalii, biashara na uwekezaji.

Vilevile, Rais Dk. Mwinyi alieleza kuridhishwa kwake na kazi kubwa inayofanywa na Mamkala ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) hususan mabadiliko ya utendaji yanayozingatia uwajibikaji na nidhamu, pia kusifu juhudi kubwa wanazofanya wafanyakazi wa mamlaka hiyo kuufanya uwanja huo kupokea wageni wengi zaidi.

Akizungumzia ukuaji wa utalii nchini, Rais alisema takriban watalii milioni mbili wanaingia nchini kila mwaka, hivyo kuna kila sababu kwa serikali kuchukua juhudi maalumu za kuimarisha viwanja vya ndege kwa miundombinu bora.

Rais Dk. Mwinyi aliahidi ujenzi wa hoteli kubwa zenye hadhi ya juu ili kuwavutia wageni wengi zaidi, hatua itakayoimarisha utalii na kuongeza mapato yanayotokana na sekta huyo muhimu kiuchumi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed alimshukuru Rais Dk. Mwinyi kwa busara na miongozo anayotoa kwa wizara hiyo ambayo imechangia maendeleo makubwa ya viwanja vya ndege nchini na kumpongeza kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwaletea maendeleo Wazanzibari.

Pamoja na kusifia kazi kubwa inayofanywa na ZAA hadi kupata tuzo za kimataifa kufuatia mabadiliko ya utendaji katika mamlaka hiyo ya utoaji wa huduma bora.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAA, Seif Abdalla Juma alisema ujenzi wa majengo ya abiria 'Terminal One' na 'Two' na kituo cha kisasa cha biashara yanagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ujenzi umefikia hatua nzuri na kuongeza kuwa umetokana na kuchakaa kwa majengo ya zamani ambayo hayaendani na mahitaji ya sasa ya mabadikilo ya viwanja vya ndege duniani.

Alisema mbali ya mabadiliko makubwa uwanjani huko, wanakusudia kuweka mfumo wa kisasa wa kuhifadhi makontena ya mizigo kwa lengo la kuendana na mahitaji na ubora wa viwanja vya sasa vya ndege duniani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***


THE JUDICIARY OF TANZANIA
IN THE DISTRICT COURT OF BIHARAMULO AT BIHARAMULO
REVISION NO: 000025005 OF 2024
CASE REFERENCE NO. 20241007100025005
AKILIMALI DAUDI...........1ST COMPLAINANT/APPELLANT/APPLICANT
MAPAMBANO JURUMANI..............2ND COMPLAINANT/APPELLANT/APPLICANT
VERSUS
EUSTACH SAHIRO......................1ST RESPONDENT
ZUHURA BRAITON...................2ND RESPONDENT
SYLIVANUS STEPHANO KASHAGAMA OF SYSKA SERVICE COMPANY LTD.....3RD RESPONDENT

NOTICE OF MENTION

TO: 1. EUSTACH SAHIRO, 2. ZUHURA BRAITON, 3. SYLIVANUS STEPHANO KASHAGAMA OF SYSKA SERVICE COMPANY LTD.

This is to notify you that the mention matter is scheduled for mention/hearing on the 31st day of December of year 2024 at 9:00 am before Hon. S.S. Mashambo – SRM.

You are required to attend in person or your advocate.
Failure to attend the matter shall proceed exparte against you.

Given under my hand and the seal of the court this 12th day of December, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
BIHARAMULO

KUPOTEA KWA CHETI



MAGRETH THADEUS KASAPILA, Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S4104/0504** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Lugoba Mwaka 2016. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/54286/2024**

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YAHAYA MUSSA MMBAGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye majina YASINI MUSSA MMBAGA namba za usajili **T176DSP** aina ya Toyota HARRIER, Chassis No. **MCU30-0002226,** Engine No. **1MZ-FE 2994.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/53444/2024**

# Kasi kesi za ubakaji, ulawiti yawashtua majaji wanawake

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Majaji Wanawake Tanzania(TAWJA) kimesema kuwa kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la kesi za ubakaji na ulawiti nchini.

Mwenyekiti wa TAWJA, Jaji wa Mahakama ya Rufani Barke Sehel alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka 25 ya kuanzishwa chama hicho yatakayofanyika Januari mwakani jijini Arusha, mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Miaka ya nyuma kesi hizi zilikuwa chache na zilikuwa zinasikika katika baadhi ya mikoa tu, lakini miaka ya hivi karibuni mikoa yote ina matukio haya na yanafanyika kwa kiwango kikubwa. Hivyo, katika maadhimisho yetu, haya ni miongoni mwa mambo ambayo tutayazungumza.

"TAWJA tunafanya jitihada kuhakikisha changamoto hizi zinatatuliwa katika nyanja mbalimbali hasa kwa kutoa elimu katika eneo la usawa wa kijinsia na mambo mengine yanayofanana na hayo," alisema.

Jaji huyo alisema suala la mirathi kwa wanawake nalo ni eneo lenye kesi nyingi hivi sasa na wanawake ndio waathirika wakubwa wanaonyimwa kurithi mali hususani wanapofiwa na wenza wao.

"Kwahiyo tunaendelea kutoa elimu kwenye jamii kwa kujengea uwezo kutambua haki zao hasa katika mirathi, talaka, haki za usawa na masuala mengineyo," alisema Barke.

Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho hayo, Sophia Wambura, alisema katika kipindi hicho cha miaka 25, TAWJA imefanikiwa kukuza hali ya usawa kwenye ngazi ya utendaji wa mahakama.

Jaji Sophia alisema tofauti na miaka ya nyuma, hivi sasa idadi ya wanawake majaji imezidi kuongezeka na kuwaongezea ari wanawake na wasichana wengi kuingia katika sekta hiyo licha ya kwamba hawajafikia kwenye ngazi ya juu ya uongozi katika eneo hilo.

Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Aisha Bade alisema miongoni mwa mambo ambayo TAWJA wameyaona ndani ya miaka hiyo 25 tangu kuanzishwa kwake, ni washtakiwa kushindwa kukidhi masharti ya dhamana.

"Pamoja na kwamba dhamana zinakuwa wazi, lakini wahusika wamekuwa wanashindwa kutimiza masharti kwa kukosa baadhi ya mahitaji kama vile wadhamini na vitambulisho, hivyo katika maadhimisho hayo tutalitolea elimu pia," alisema Aisha.

Maadhimisho hayo yatashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo majaji na mahakimu wanawake kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, wadau kutoka mashirika ya kimataifa ikiwamo UN Women, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF).

Kwa mujibu wa Ripoti ya Takwimu za Msingi Tanzania iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2023, matukio ya ubakaji na ulawiti yanayoripotiwa kwenye vituo vya polisi nchini yameongezeka kutoka 23 kwa siku mwaka 2022 hadi kufikia 31 siku mwaka 2023.

Takwimu hizo pia zinaonesha ulawiti umeongezeka zaidi ya mara mbili mwaka 2023 hadi kufikia matukio 2,488 kulinganishwa na kesi 1,205 zilizoripotiwa mwaka 2020.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akikagua miundombinu ya ujenzi wa daraja la Simiyu jana linalounganisha mikoa ya Mwanza, Simiyu na Mara ambalo ujenzi wake utagharimu Sh. bilioni 48.7 hadi kukamilika kwake. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# LATRA: Kateni tiketi za elektroniki mlipwe fidia dharura ikitokea safarini

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo amewataka abiria kukata tiketi za kielektroniki zenye taarifa zao sahihi wanaposafiri na mabasi ya masafa marefu ili iwe rahisi kufuatilia bima kwa ajili ya kuwafidia endapo itatokea dharura safarini.

Suluo amesema tayari mfumo huo wa tiketi unaotumika umeunganishwa na LATRA pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hivyo ni rahisi kwao kufuatilia endapo abiria watapata matatizo njiani.

Alisema hayo juzi baada ya ukaguzi wa kushtukiza aliofanya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwenye Kituo cha Mabasi Magufuli, Dar es Salaam kwa lengo kuangalia hali ya usafiri na kuimarisha usalama wa vyombo vya usafiri katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Alisema ukaguzi huo uliangalia zaidi utekelezaji masharti ya leseni, ikiwamo matumizi sahihi ya Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i- Button), matumizi sahihi ya tiketi mtandao pamoja na Jeshi la Polisi kupima kiwango cha ulevi kwa madereva wa mabasi ya masafa marefu.

"Ni jukumu letu kuhakikisha mabasi yapo na abiria wanasafiri kwa nauli ambayo tumeipanga, na tumebaini kuwa hali ni nzuri na abiria wote wamesafiri usiku na asubuhi ya leo (juzi) tumekagua na kuona tiketi zimetolewa japo kuna tatizo dogo kwa wale abiria ambao wanashuka njiani.

"Mfano abiria wanaopanda magari yanayokwenda Musoma na kushuka Morogoro hawapewi tiketi na hii ni hatari kwa usalama wao," alionya.

Aliwataka abiria kutumia mfumo wa PIS unaopatikana katika tovuti ya LATRA ili kufahamu mwendokasi wa basi na endapo watabaini ni hatarishi, wapige simu bila malipo kwa LATRA kupitia namba 0800110019 au 0800110020 saa 24 siku zote.

Alisema LATRA inatumia mfumo wa kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kufuatilia kwa ukaribu mabasi yote na kupitia i-Botton wanaona mwenendo mzima wa dereva, na kuwaomba madereva kuendesha kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Suluo pia alitoa nafasi kwa wasafirishaji wenye mahitaji ya ziada kwa kuwataka wawasilishe maombi kwa mamlaka hiyo, kwa magari ambayo yana siti zaidi ya 40 ili kupatiwa vibali vya kutoa huduma ya usafirishaji kwa muda mfupi.

"Jambo la muhimu ni msafirishaji awe amekidhi masharti ya leseni ikiwamo kufunga mfumo wa VTS, awe na mfumo wa kutolea tiketi na dereva anayesafiri awe amethibitishwa na mamlaka.

"Hadi sasa mamlaka imetoa vibali vitatu tu kwa mkoa wa Arusha na manispaa ya Moshi na hali hii ni matokeo mazuri ya safari za saa 24 ambapo kwa sasa hali ya usafiri imekuwa salama na hakuna msongamano wa abiria katika stendi vya mabasi," alisema.

# Waziri aagiza kufungwa viwanda na maduka yenye nyavu zisizofaa

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji ameagiza kufungwa kwa viwanda na maduka yote yanayojihusisha na uuzaji nyavu zisizofaa kwenye shughuli za uvuvi ikiwa ni hatua ya kukomesha uvuvi haramu nchini.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara yake mkoani Mara baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji shughuli za uvuvi mkoani humo iliyobainisha kuwapo changamoto kubwa ya uvuvi haramu.

"Hizi nyavu na nyenzo nyingine za uvuvi haramu kuna mahali zinatengenezwa na kuuzwa ndipo zinawafikia wavuvi wetu, hivyo ni lazima tuanzie huko kwenye msingi kabla hatujawashughulikia wavuvi," alisema.

Dk. Kijaji alisema moja ya majukumu yake makubwa wakati wote atakaohudumu kwa nafasi yake ni kuhakikisha anarejesha hali ya upatikanaji samaki nchini kama ilivyokuwa awali ili kuokoa viwanda vya kuchakata samaki vilivyomo nchini.

Alisema serikali itaweka mkakati wa kuzuia uingizaji zana za uvuvi kutoka nje kupitia mipaka ya nchi, Kwa kuanzia, udhibiti utaanzia katika mpaka wa Tunduma ulioko mkoani Songwe.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi alitangaza awamu nyingine ya kupambana na uvuvi haramu mkoani mwake itakayoanza Januari mwakani. Aliwataka wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo kuacha mara moja huku akiwatahadharisha kutomlaumu pindi atakapoanza kutekeleza operesheni hiyo.

"Mtu anayefanya vitendo vya uvuvi haramu ni mhujumu na sisi jeshini mhujumu hatumpetipeti, bali tunamshughulikia ipasavyo," Mkuu wa Mkoa alionya.

Dk. Ashatu amefanya ziara yake ya kwanza kikazi mkoani Mara tangu alipoapishwa kushika wadhifa huo. Akiwa mkoani humo, waziri huyo amefanya vikao kazi na wataalamu na watendaji wa serikali na kutembelea vizimba vya kufugia samaki vilivyotolewa na serikali kwa mkopo wa masharti nafuu kwenye eneo la Lake Side.


MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONEERS (T) LTD.

**NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONEERS LTD**, kwa idhini tuliyopewa na **MTEJA WETU**, tunatoa notisi ya siku kumi na nne ya kulipa dhamana itauzwa kwa njia ya **MNADA WA HADHARA,** mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa 6:00 mchana na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | JOSEPH PAUL LEYARO | HATI NAMBA: 2435 PLOT NO. 2, Kijiji cha Ikirevi, jijini Arusha. | Jumatatu, 6/01/2025 kuanzia saa 06:00 mchana |
| | | HATI NAMBA: 25806 PLOT NO. 621, Sombetini, Manispaa ya Arusha. | Jumatatu, 6/01/2025 kuanzia saa 06:00 mchana |
| | | HATI NAMBA: 23931 PLOT NO.790, Themi, Manispaa ya Arusha. | Jumatatu, 6/01/2025 kuanzia saa 06:00 mchana |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi, piga simu na: **0752722222**

## TANGAZO

# DERM group

**Derm Group (T) Ltd and its subsidiaries** wishes to inform its esteemed clients and business partners that our offices will be closed during the festive season with effect from **Saturday, 21st December 2024.**

**Business will resume on Monday 6th January 2025**.

Our site operations and regional offices in **Kagera, Dodoma, Geita, Songwe, Tanga, Mbeya, Kigoma, Dar es salaam and Shinyanga** shall not be affected by this closure.

Any inconveniences caused is highly regretted.
We would like to thank all our clients and business partners for their continued patronage of our services throughout the year.

"We wish you all a Merry Christmas and prosperous, productive and innovative 2025".



SKYLINE PROPERTIES LTD

Derm Elevators

dermgrouptz
info@derm.co.tz
www.derm.co.tz

218304001

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Karia kuendelea urais TFF, sawa ila atuondolee madudu haya

**KUNA** asilimia kubwa rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, akachaguliwa tena kuendelea kuongoza kwa kipindi kingine, baada ya wajumbe wengi kuonekana kuridhishwa na utendaji wake.

Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu na rais wa Klabu ya Yanga, Injinia Hersi Said, wao waliuomba Mkutano Mkuu uliofanyika Moshi, Kilimanjaro, Jumamosi, kumpitisha moja kwa moja kutokana na kuridhishwa na kazi kubwa aliyoifanya kwa miaka saba aliyokaa madarakani.

Hata hivyo, Makamu wa Kwanza wa rais, Athumani Nyamlani, alijibu kuwa njia bora ya kufanya hivyo ni wanachama wote wa shirikisho hilo kumwekea dhamana mara akishachukua fomu ya kuwania urais na si kumpitisha moja kwa moja kwa kutofanya uchaguzi kama viongozi wa Simba na Yanga walivyoshauri.

Kwa ujumla, tunathamini mchango wa viongozi wa klabu hizo kongwe, lakini tunapongeza uamuzi wa Nyamlani wa kusimamia demokrasia kuwa uchaguzi ni lazima ufanyike, kwani vyama vinavyosimamia demokrasi uchaguzi huwa ni suala la kikatiba.

Tukirudi upande wa Karia ni lazima apongezwe kwa kiasi kikubwa kurudisha heshima ya shirikisho hilo na kulifanya kuaminika na taasisi kubwa na kampuni mbalimbali nchini tofauti na miaka ya nyuma.

Hakuna asiyejua kuwa taasisi ya mpira wa miguu, hasa wakati huo ikiitwa Chama cha Mpira Miguu nchini (FAT), ilikuwa haiheshimiki, kukubalika na wala kuaminika.

Ni chama kilichokuwa kikikumbwa na migogoro ya mara kwa mara kwa viongozi wenyewe kwa wenyewe na hata kwa taasisi zingine. Pamoja na kwamba mpira wa miguu ulikuwa ukipendwa sana, lakini bado haukuwa kwenye mifumo sahihi na ya kisasa kama hivi leo.

Huko nyuma tuliona hata pesa za viingilio zikichukuliwa kwenye viroba na kupelekwa benki au kulala ofisini. Hata wachezaji walikuwa wakisajiliwa kwa kuwekewa lundo la noti mezani.

Leo hii imekuwa historia. Kila kitu kinafanyika kwenye mifumo sahihi ya kipesa, kama vile benki na mifumo mingine ya kiserikali.

TFF imekuwa ni Shirikisho linaloaminika na kampuni nyingi iwe ndani na nje ya nchi, hivyo kuzivutia kudhamini ligi na michuano mingine.

Kabla ya Karia kuingia madarakani, Tanzania ilikuwa imefuzu AFCON mara moja tu, lakini wakati wa utawala wake imefanya hivyo mara tatu kiasi kwamba kutinga hatua hiyo kwa sasa kwa Taifa Stars si habari kubwa tena.

Klabu kama Simba na Yanga zimefanya vizuri sana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho na kwa sasa kuwa moja ya nchi inayoogopewa kwenye mashindano mbalimbali ya klabu barani Afrika, hapo huwezi kukwepa juhudi za Karia. Ligi ya Tanzania kwa sasa ipo nafasi ya sita kwa ubora. Timu za Vijana nazo na za wanawake huwezi kuziacha kwa kufanya vema. Yote hii ni chini ya utawala wake.

Pamoja na yote bado haiwezekani apitishwe tu moja kwa moja bila uchaguzi. Tuna uhakika kuwa atachaguliwa kuendelea kuwa rais wa TFF kwa hiki kinachoonekana, lakini kwa sasa kuna vitu anavyotakiwa kuviondoa ili amalize kwa amani na kuwa kiongozi wa kukumbukwa.

Kwanza ni kuifanya ligi ya Tanzania kuwa na waamuzi bora, kuanza kutumika kwa VAR, pamoja na kuondoa kampuni moja kudhamini klabu zaidi ya moja.

Yatasemwa yote, lakini hili ni doa kwenye mpira wa Tanzania. Mdhamini aliyewekeza kwenye timu moja kudhamini tena timu zingine ni moja ya mambo ambayo wadau wengi wa soka wanalalamikia na ni lazima lipatiwe ufumbuzi kwa kuondolewa kitu kama hicho.

Haya ndiyo mambo ambayo Karia anapaswa kuyaondoa kuanzia msimu ujao ambao atakuwa akianza muhula mpya wa uongozi wake endapo akichaguliwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Makocha, viongozi hatutaki visingizio mwisho wa msimu

Na Adam Fungamwango

**HUU** ni wakati wa usajili wa dirisha dogo, ambalo hufunguliwa kwa lengo la kuzisaidia klabu kusajili wachezaji wa kuongeza nguvu kwenye vikosi vyao.

Walioleta mfumo huu walikuwa na lengo la kuwasaidia viongozi na makocha kurekebisha au kuimarisha vikosi vyao baada ya mechi za mzunguko wa kwanza.

Wakati mwingine timu inakuwa imeshaanza kuwa na majeruhi, au baadhi kushuka viwango, lakini inawezekana usajili wa mwanzo wa msimu haukukidhi matarajio, hivyo ni kipindi cha kuziba mapengo ambayo yalionekana wakati mechi za mzunguko wa kwanza zikiendelea.

Tumeona baadhi ya makocha ambao walijiunga na timu mara baada ya walimu wa mwanzo kutimuliwa wakilalamika kukuta kuna mapungufu makubwa kwenye vikosi vyao.

Hata baadhi ya viongozi nao wameonekana kuzungumzia mapungufu ya vikosi vya wakati michezo ikiendelea.

Mfano, mmiliki wa Fountain Gate, Japhet Makau, amebainisha wazi kuwa kikosi chao pamoja na kwamba kina safu bora ya ushambuliaji, lakini kimeonekana kuwa na matatizo upande wa ulinzi.

Akabainisha kuwa kipindi hiki watafanya kila njia ili kusajili wachezaji ambao watakuja kuimarisha ukuta.

Kocha Mkuu wa KenGold, Omari Kapilima, naye ameilalamikia safu yake ya ulinzi kuwa haipo vizuri, akawa analisubiri dirisha dogo ili kufanya usajili kutatua tatizo hilo.

Makocha kama Juma Mwambusi wa Coastal Union na Juma Mgunda wa Namungo FC nao wameelezea kuwa watafanya usajili ili kufanya maboresho kwenye vikosi vyao, kwani wamevikuta kuna maeneo vina mapungufu.

Hii inaonesha kuwa kuna uhitaji mkubwa wa wachezaji kipindi hiki cha dirisha dogo.

Ingawa mara nyingi inasemekana katika kipindi hiki huwa hakuna wachezaji wazuri sana wanawekwa sokoni na klabu nyingi hazipendi kuuza wachezaji kipindi hiki kwani huwa kwenye ligi na michuano mingine, lakini wale wa kuziba mapungufu machache yaliyopo wanapatikana.

Si kwenye Ligi Kuu ya soka la wanaume tu, hata katika timu ya soka wanawake pia zipo timu zinahitaji kufanya usajili kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao.

Mfano, Yanga Princess inaonekana ina shida kwenye upande wa kiungo mshambuliaji na straika wa kupachika mabao, Simba Queens ikiwa na tatizo kubwa la golikipa, pamoja na straika mmoja wa kumsaidia Jentrix Shikangwa, hasa baada ya kuondoka kwa Aisha Mnunka, JKT Queens ikitakiwa kuongeza kiungo mshambuliaji wa kupiga pasi za mwisho na zingine ambazo zinaonekana zina mapungufu makubwa zaidi ya hizi nilizozibainisha.

Ni wakati wa viongozi wa klabu kuwaunga mkono makocha na kuwaletea kile ambacho wanakihitaji na si kile ambacho wao wanapenda kukileta.

Kuna baadhi ya viongozi husajili wachezaji kwa matakwa na mapenzi yao binafsi, kocha anataka beki wa kati, lakini wanasajili mastraika kwa sababu tu ni mchezaji mwenye jina ili apate sifa.

Matokeo yake ligi inaisha timu haipati matokeo mazuri anayefukuzwa ni kocha kwa kuonekana hajafanya vizuri, kumbe tatizo lipo kwa viongozi ambao wameshindwa kumletea kocha wachezaji anaohitaji.

Kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili ni wakati wa viongozi kuwasikiliza makocha wanataka nini, kuwatekelezea wanachohitaji, ili kuwahukumu kwa haki mwishoni mwa msimu.

Binafsi, ningependa hukumu ya haki mwishoni mwa msimu, kama viongozi wamevurunda kwenye usajili basi wajitathimini wenyewe na kama kocha ameletewa kila kitu na ameshindwa, basi awajibishwe.

Nisingependa kuona viongozi wakiwa na visingizio vingi mwishoni mwa msimu na kumalizia kwa kuwabebesha lawama makosa, au makocha kuwanyoshea vidole viongozi ambao wachezaji walionao na wakashindwa kuwapa walichokihitaji.

Timu zisajili vizuri, hatutaki visingizio mwishoni mwa msimu.

## Ashikiliwa kwa tuhuma kumuua mzazi mwenzake, kutupa mwili barabara kuu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha linamshikilia mkazi wa Makumira wilayani Arumeru, John Maganga (26) kwa tuhuma za mauaji ya Safina Emanuel (19), mama lishe na mkazi wa Magadirisho wilayani humo.

Akitoa taarifa hiyo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Justine Masejo, alisema mwili wa marehemu ulikutwa maeneo ya Makumira, kando ya barabara ya Moshi-Arusha.

Kamanda Masejo alisema kuwa baada ya kupata mwili huo, walianza upelelezi na kufanikisha kumkamata mtuhumiwa huyo ambaye ni mzazi mwenza wa marehemu.

"Baada ya kumkamata, alikiri kuhusika na mauaji hayo Desemba 19 mwaka huu na tulipoendelea kumhoji, alitueleza namna ambavyo alificha mwili huo," alisema.

Kamanda Masejo alisema wanaendelea na upelelezi wa tukio hilo na utakapokamilika taratibu nyingine za kisheria zitafuata dhidi ya mtuhumiwa huyo.

Alisema jeshi hilo litaendelea kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria dhidi ya watu wote watakaojihusisha na vitendo vya uhalifu.

Pia aliwaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za wahalifu na uhalifu ili washughulikiwe.

**"Baada ya kumkamata, alikiri kuhusika na mauaji hayo Desemba 19 mwaka huu na tulipoendelea kumhoji, alitueleza namna ambavyo alificha mwili huo," alisema.**



Waziri wa Mambo ya Ndani, Innocent Bashungwa akimjulia hali mmoja wa abiria waliolazwa katika hospitali teule ya Biharamulo baada ya kupata ajali ya basi la abiria katika eneo la Kabukome katika kata ya Nyarubango wilayani Biharamulo mkoani Kagera juzi. **PICHA: RESTITUTA DAMIAN**

# Majaliwa aagiza TANROADS iongeze kasi ya ujenzi wa daraja la mita 175

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka viongozi wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Mwanza waongeze kasi ya ujenzi wa daraja la Simiyu lililoko wilayani Magu kwenye barabara kuu ya Mwanza-Musoma ili likamilike kwa wakati.

Ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa mita 175, upana wa mita 12.3 na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa tatu, ulianza Oktoba 30 mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Aprili 29 mwakani. Daraja hilo linaunganisha mikoa ya Mwanza na Mara.

Akizungumza na wananchi waliofika kwenye daraja hilo juzi, Waziri Mkuu alisema wilaya ya Magu ina fursa nyingi za kiuchumi na kukamilika kwa ujenzi huo kutafungua milango kwa wana-Magu.

"Magu ni wilaya ya fursa kiuchumi, Magu ni pumulio la Jiji la Mwanza. Je, wana-Magu mmejipangaje kuzikamata hizo fursa? Ninawasihi jengeni vituo vya mabasi, hoteli, maeneo ya vyakula na burudani.

"Boresheni miundombinu ya usafirishaji ili mtu akitoka Mwanza awe na uhakika kuwa anaweza kurudi kwa haraka bila shida yoyote," Waziri Mkuu aliagiza.

Akitoa taarifa kwa Waziri Mkuu kuhusu ujenzi wa daraja hilo, Mhandisi Katetula Kaswaga kutoka TANROADS Makao Makuu, alisema mradi huo utakaogharimu Sh. bilioni 48.7, unafadhiliwa na serikali kwa asilimia 100.

"Mradi unajengwa na mkandarasi China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) chini ya usimamizi wa Mhandisi Mshauri ambaye ni TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU). Kazi iliyofanyika hadi sasa imefikia asilimia 35," alisema.

Awali Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya alisema kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo, kutasaidia kupunguza ajali na msongamano kwa kiasi kikubwa kwa kuwa daraja la zamani lilikuwa na njia moja. Linalojengwa litakuwa na njia mbili.

Alisema ujenzi wa daraja la Simiyu ni miongoni mwa miradi mikubwa nchini ambayo imelenga kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

"Daraja hili lilijengwa kabla ya uhuru, lilikuwa limebakia peke yake kwenye barabara kuu za nchi nzima. Serikali ya awamu ya sita ilishaamua kuondoa madaraja kama hayo kwenye barabara kuu nchini.

"Tungeliacha liendelee kuwapo, lingeleta changamoto ya foleni kwenye magari ya mizigo yanayokuja nchini na kwenda kupita kwenye daraja la Kigongo-Busisi," alifafanua.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa daraja la Sukuma katika kata ya Ng'haya ambalo linaunganisha wilaya za Magu na Bariadi.

Daraja hilo lenye urefu wa mita 70, upana wa mita 11.3 na barabara unganishi za kilomita 2.3, linajengwa na mkandarasi mzawa ambaye ni Mumangi Construction Co. Ltd. Hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 24 na utagharimu Sh. bilioni 10 hadi kukamilika kwake.

Naibu Waziri Kasekenya alisema ujenzi wa daraja hilo ni utekelezaji moja ya mikakati ya serikali ya kuboresha sekta ya miundombinu nchini na kwamba kukamilika kwa daraja hilo kutarahisisha usafiri na usafirishaji watu na bidhaa, na pia kuchochea uzalishaji katika sekta za kilimo, madini na viwanda.

Alisema daraja litakapokamilika na barabara hiyo ikaanza kutumika, itafupisha safari za kwenda mkoani Mara. Alisema barabara hiyo itakuwa fupi, kilometa 74 tu kwenda Mara," alisema.

Katika ziara hiyo ya siku moja, Waziri Mkuu alifuatana na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Ujenzi, Kasekenya, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Zainab Katimba, wabunge wa Magu, Sengerema, viti maalum na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Mwanza.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# IGP Wambura afumua uongozi Kikosi cha Usalama Barabarani

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura amefanya mabadiliko madogo kwa wakuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani.

Katika mabadiliko hayo amemhamisha Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Ramadhani Ng'anzi kutoka Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabaarani Tanzania kwenda Makao Makuu ya Upelelezi Dodoma kuwa Mkuu wa Kitengo cha Makosa ya Maadili ya Jamii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na DCP David Misime, Msemaji wa Jeshi la Polisi, nafasi ya DCP Ng'anzi inachukuliwa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) William Mkonda ambaye alikuwa Mkuu wa Usalama Barabarani Kanda Maalum Dar es Salaam.

**IGP pia amemhamisha aliyekuwa Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Boniphace Mbao kutoka Dodoma kwenda kuwa Mkuu wa Usalama**

IGP pia amemhamisha aliyekuwa Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Boniphace Mbao kutoka Dodoma kwenda kuwa Mkuu wa Usalama Barabarani Kanda Maalum Dar es Salaam.

Vilevile, aliyekuwa Mkuu wa Elimu kwa Umma Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Michael Deleli amemhamishia Makao Makuu ya Polisi Dodoma kuwa Kaimu Mkuu wa Maadhimisho ya Kitaifa.

Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Nassoro Sisiwaya aliyekuwa Mkuu wa Operesheni Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania amemhamishia Mkoa wa Kilimanjaro kwenda kuwa Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Kilimanjaro.

Hakuna sababu iliyotajwa kuchangia mabadiliko hayo. Lakini yamefanywa kipindi ambacho kunaripotiwa ajali za barabarani zinazogharimu maisha ya makumi ya wananchi.

# Sheria kutambua wanataaluma uchukuzi yaja

Na Grace Gurisha

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masuala ya uchukuzi iko katika hatua za kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Bodi ya Uchukuzi kwa lengo la kuwatambua na kuwasajili wanataaluma hao.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile alisema hayo wakati wa mahafali ya 40 ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) mwishoni mwa wiki, akiongeza kuwa bodi hiyo itakuwa na jukumu la kusimamia weledi na maadili ya wataalamu wa uchukuzi Tanzania Bara.

Alisema uanzishwaji bodi hiyo una lengo la kuhakikisha kazi zote za usafirishaji zinasimamiwa na watu wenye taaluma stahiki.

Akizungumzia kuhusu NIT, Kihenzile alisema serikali itaendelea kukiwezesha chuo hicho kwa kuboresha miundombinu yake ya kufundishia ili kuhakikisha kinatimiza majukumu yake ya kuandaa wataalamu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika sekta ya uchukuzi kwa maendeleo endelevu ya taifa.

Kihenzile alitoa rai kwa wadau mbalimbali wa usafiri na usafirishaji kuunga mkono jitihada za chuo katika kuwapatia nafasi za mafunzo kwa vitendo wanafunzi na kuendeleza ubunifu unaozalishwa chuoni ili utumike kwa maendeleo ya nchi.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwamo NIT, iko katika hatua za kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Uchukuzi.

"Lengo ni kuwatambua, kuwasajili na kusimamia weledi wa maadili ya wataalamu wa uchukuzi Tanzania Bara ili kuhakikisha kwamba kazi zote za usafirishaji zinasimamiwa na watu wenye taaluma stahiki," alisema.

Awali Mkuu wa NIT, Dk. Prosper Mgaya alisema katika mahafali hayo wahitimu 4,176 wametunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali. Kati yao, wanaume ni 2,581 na wanawake 1,595.

Akizungumzia changamoto, alisema chuo kimekuwa na mikakati ya kukabiliana nazo zikiwamo za miundombinu na upungufu wa rasilimali watu sambamba na ongezeko la udahili wa wanafunzi kwa kuweka mikakati mbalimbali.

Alisema sambamba na mabweni, chuo kinajenga ofisi, madarasa na karakana, majengo matatu yanajengwa na yanatarajiwa kukamilika Februari mwakani. Ujenzi unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) kupitia mradi wa EASTRIP.

Dk. Mgaya alisema chuo pia kinaanzisha kampasi mpya mkoani Lindi na Kilimanjaro ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika kampasi ya Dar es Salaam na kuhusu rasilimali watu, wanaendelea kuomba vibali vya ajira serikalini ili kupunguza matumizi ya walimu/ wahadhiri wa muda.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam akiwa amefunga viroba vya mkaa kwa ustadi kwenye baiskeli yake eneo la Kinyerezi juzi. Rais Samia Suluhu Hassan anahamasisha utumiaji wa majiko ya gesi kwa ajili ya kupikia ili kupunguza matumizi ya mkaa ikiwa ni pamoja na kulinda mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Wapeni elimu ya sheria viongozi wa ngazi za chini'

Na Sabato Kasika

MKURUGENZI wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni amewataka watumishi wa Dawati la Msaada wa Kisheria Jiji la Dar es Salaam, kutenga muda wa kutosha ili kukutana na viongozi wa ngazi za chini kuwapa elimu kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria ili wawe na uelewa wa kuwasaidia kutoa uamuzi sahihi kwenye mashauri ya kisheria.

Seleman Bishagazi ametoa rai kwa watumishi hao juzi baada ya kumtembelea kituoni huko kwa nia ya kujitambulisha ikiwa ni sehemu ya maandalizi yao kutoa elimu ya kusaidia jamii kujua haki zao za kisheria wanapofikisha malalamiko kwa viongozi au wanapotekeleza majukumu yao.

Bishagazi alisema katika ngazi za chini kuna migogoro mingi ikiwamo ya ardhi, mirathi, ndoa na ukatili wa kijinsia, na kwamba watumishi hao hawana budi kushuka chini hadi kwa viongozi wa ngazi hizo kuwapa elimu kwa kuwa wengi wao hawana uelewa wa kutosha wa mambo ya kisheria.

"Tuna viongozi wa mabaraza ya ardhi ya kata wanapelekewa migogoro ya ardhi, hawajui sheria. Inakuwa vigumu kutatua migogoro, hivyo ni vyema mtenge muda wa kuja kuwasaidia," alisema Bishagazi.

Aliongeza kuwa hata viongozi wa serikali za mitaa wanapaswa kupata elimu ya mambo ya kisheria ili nao wawasaidie wananchi wanapofika kwao kupata msaada wa mambo mbalimbali yakiwamo ya kisheria.

"Huku chini kuna migogoro mingi, hivyo ni vyema mkaandaa ratiba ya kuja kuwapa elimu ya sheria angalau viongozi wawe na uelewa wa kutatua migogoro au kuwaelekeza wananchi waende wapi wapokuwa na tatizo fulani," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Dawati la Msaada wa Kisheria Jiji la Dar es Salaam, Innocent Masanja, alisema kuwa yeye na wenzake watalifanyia kazi ombi hilo.

Alikiri kuwa kuna changamoto nyingi katika jamii ambazo nyingine zinatokana na kutoelewa sheria na kusababisha kuwapo migogoro mingi isiyoisha.

"Tulichokuja kufanya ni sehemu ya kampeni iitwayo Mama Samia Legal Aid inayolenga kuwezesha wanajamii kujua haki zao za kisheria, hivyo tutaendelea kushirikiana nanyi na tutafanyia kazi ombi na ushauri wa mkurugenzi wa kituo hiki," alisema Masanja.





## Maganga ataka weledi utekelezaji majukumu OSHA

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WATUMISHI wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), wametakiwa kuzingatia weledi katika kutekeleza jukumu lao la msingi ili kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma bora.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mary Maganga, alitoa maelekezo hayo, alipokuwa akifunga Kikao cha Tatu cha Baraza la Tano la Wafanyakazi wa OSHA kilichohitimishwa (Desemba 19, 2024) jijini Arusha.

Akiwasilisha hotuba yake ya kufunga kikao tajwa, Katibu Mkuu, Mary Maganga, alisema kwa kuzingatia wajibu wa OSHA wa kuzuia ajali, magonjwa na vifo mahali pa kazi, utekelezaji wa majukumu husika unahitaji weledi wa hali ya juu.

"Nitumie fursa hii kuwakumbusha kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia weledi, kuwa na nidhamu na kuepuka visingizio vya aina yoyote katika kutekeleza majukumu yenu ya kila siku.

"Tukifanya kazi kwa weledi, tutaepuka kuwasababishia machungu zaidi wananchi tunaowahudumia ambao wakati mwingine wanakuwa wamekumbwa na matatizo kama vile ajali mahali pa kazi, kupoteza wapendwa wao au kuharibiwa mali zao," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa TUGHE na vyama vingine vya wafanyakazi kufanya jitihada kuzuia migogoro baina ya waajiri na wafanyakazi mahali pa kazi badala ya kusubiri kutatua migogoro inayotokea.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema kikao cha tatu cha Baraza la Wafanyakazi wa OSHA kilikuwa maalumu kwa ajili ya kutathmini utendaji wa taasisi kwa mwaka 2023/2024 pamoja na robo ya kwanza ya mwaka 2024/2025.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE), Mudathir Athuman na mwakilishi wa wafanyakazi wa OSHA, Alfredy Shechambo, walipongeza Menejimenti ya OSHA kwa kuandaa vikao vya mabaraza ya wafanyakazi kwa mujibu wa sheria za nchi pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi yenye lengo la kuimarisha utendaji wao.

# TCB yatangaza wazalishaji bora wa kahawa, kuiwakilisha nchi kimataifa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BODI ya Kahawa Nchini (TCB), imewatangaza rasmi wazalishaji wa kahawa bora, watakaopeperusha bendera ya Tanzania katika mkutano wa kimataifa na maonesho ya kahawa bora Afrika, yatakayofanyika Februari 26 hadi 28 mwakani.

Tanzania itakuwa mwenyeji wa mikutano miwili mikubwa ya kimataifa, ikiwamo ule wa nchi wanachama wa Chama cha Wazalishaji wa Kahawa Afrika, utakaohusisha nchi 55 zinazozalisha kahawa Afrika.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika Mji wa Moshi, Kilimanjaro, wakati wa hafla ya kukabidhi vikombe na vyeti kwa washindi wa mashindano ya uzalishaji wa kahawa bora, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Kajiru Kisenge alisema:

"Tunashuhudia leo kazi kubwa iliyofanywa na wakulima wetu na wazalishaji wa kahawa nchini. Kwa niaba ya TCB, ambao tuliandaa mashindano haya kwa ushirikiano na Chama cha Kahawa Bora Africa (AFCA), tunatoa pongezi za dhati kwa kila mmoja aliyeshiriki kwa kuwasilisha sampuli.

"Washindi ambao ni wazalishaji wetu wa kahawa, wamekuwa ni mfano wa kujituma, wamekuwa wabunifu, wamekuwa na uvumilivu na wamekuwa wakiendelea kutimiza wajibu wao wa kuzalisha kahawa bora.

Pia, mashindano haya yamekuwa ni fursa ya kuonesha ubora wa kahawa yetu na kuipeleka kahawa yetu katika soko la kimataifa. Kwa sababu kufanyika kwa mashindano haya ni njia ya kuzipeleka kahawa zetu kwenye mashindano ya kimataifa ambayo yatafanyika baadaye mapema mwakani."

Jaji Kiongozi wa mashindano hayo aliyeteuliwa na AFCA, Grace Mukayisenga (Rwanda), alisema mashindano hayo yamehusisha kundi la kahawa ya robusta, ambayo inalimwa kwa asilimia kubwa Mkoa wa Kagera na Natural Arabika's (Arabika ngumu), ambayo hupitia hatua isiyohusisha maji kabisa au kwa kiwango kidogo kabisa kwenye hatua ya awali ya uchakataji kwa ngazi ya mkulima.

> **"Washindi ambao ni wazalishaji wetu wa kahawa, wamekuwa ni mfano wa kujituma, wamekuwa wabunifu, wamekuwa na uvumilivu na wamekuwa wakiendelea kutimiza...**

Wakati kundi jingine, ni la Washed Arabika's (kahawa laini) zinazohusisha maji katika maandalizi yake ya awali, ambayo yanafanyika katika ngazi ya mkulima, wakati wanaiandaa nyumbani kwa kuosha na kuvundika.

Alimtaja mshindi wa kwanza katika kundi la Natural Robusta, kuwa ni Ubumwe Company Ltd (Ngara, Kagera), wa pili Karagwe Estate (Kagera) na wa tatu, Karagwe District Co-Operative Union Ltd (Kagera).

Aidha katika kundi la Arabika Naturals, mshindi wa kwanza ni Wakulima wa Mara (Mara), mshindi wa pili ni Burka Coffee Estate na wa tatu ni Finagro Plantations (zote za Arusha).

Wakati kundi jingine ni la Washed Arabika's, ambalo mshindi wa kwanza ni Finagro Plantations (Arusha), mshindi wa pili ni Amkeni Gourmet Coffee Group na mshindi wa tatu, ni Mwika North East Amcos (zote za Kilimanjaro).

Baada ya mashindano hayo, mmoja wa washindi, Jasson Mpita, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Ubumwe Ltd, alisema wanaishukuru menejimenti ya TCB, ambao wamekuwa washauri wakuu katika jambo hilo.



Prosper Tesha Mkurugenzi wa moja ya kampuni inayochimba madini ya vito katika kijiji cha Mundarara wilaya ya Longido mkoani Arusha akimsaidia mjasiriamali, Nembulis Laizer anayejitafutia riziki yake kwa kugonga mawe yanayosadikiwa kuwa na madini aina ya Ruby alipotembelea eneo hilo hivi karibuni. **PICHA: MARY MARGWE**

# Bandari tatu kuboreshwa miundombinu ya reli kisasa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imepanga kujenga miundombinu ya reli ya kisasa katika bandari tatu nchini, ili kuongeza ufanisi wa usafirishaji mizigo na kuondoa msongamano usio wa lazima.

Kwa mujibu wa Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema miundombinu hiyo itajengwa bandari za Dar es Salaam, Mwanza na Tanga.

Prof. Mbarawa alidokeza hayo juzi, alipotembelea na kukagua Bandari ya Tanga.

"Bandari yeyote ile bila kuwa na usafiri wa reli, msongamano unakuwa mkubwa zaidi linapokuja suala la kupakia mizigo. Nitahakikisha miundombinu ya reli ya kisasa inajengwa ili kuondoa misongamano na vilevile kuhakikisha bandari hizo zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Alibainisha bandari yoyote ili ifanye kazi kwa ufanisi ni lazima kuwe na miundombinu ya usafiri ambayo ni reli na barabara, lakini usafiri wa reli ni rahisi sana ukilinganisha na usafiri mwingine wowote.

"Bandari zetu zote kuanzia ya Dar es salaam, Mwanza na hapa Tanga, nitahakikisha miundombinu ya reli ya kisasa inajengwa ili kuondoa msongamano na vilevile kuhakikisha bandari hizo zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa,

"Najua hapa miundombinu ipo ila ina tatizo, nitahakikisha kwamba reli inafanya kazi kuja bandari lakini pia kushirikiana na bandari zingine na kwamba ufanisi unakuwa mkubwa zaidi kuliko awali katika kupakia na kushusha mizigo" alisema.

Pamoja na mambo mengine, alisema serikali ina mpango wa kuendelea kufanya maboresho zaidi katika Bandari ya Tanga, ili kuongeza mapato zaidi kutoka Sh. bilioni 100 za sasa na kufikia Sh. bilioni 400 kwa mwaka.

Prof. Makame Mbarawa, alisema serikali itaongeza ujenzi wa gati nyingine yenye urefu wa mita 350 zaidi ambazo zitakamilisha mita 750 pamoja na mita 400 za uboreshwaji wa awali.

Waziri Mbarawa, alisema kuwa maboresho hayo yanafanyika katika bandari zote nchini, ambapo wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari nchini (TPA) wanatekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.



# Wananchi wakodi nyumba kuwa kituo cha polisi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUKITHIRI kwa vitendo vya uhalifu katika kata ya Mhongolo Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, kumewalazimu wananchi kuchanga na kukodisha nyumba kwa ajili ya kituo cha polisi ili kudhibiti vitendo hivyo.

Wakisimulia hali ya usalama katika eneo hilo wakati wa uzinduzi wa kituo hicho, baadhi ya wananchi, akiwemo Sharifu Said alisema kumekuwepo na vibaka, wanaoingia kwenye makazi yao nyakati za usiku na kuwaibia.

Alisema wakati mwingine vibaka hao wamekuwa wakivamia maduka na kupora, kwamba wengi wao wanatumia dawa za kulevya.

Alisema kituo hicho kitawasaidia kuwadhibititi wahalifu hao na kuwaondolea hofu ya kupoteza biashara zao, kwani walikuwa wakilazimika kufunga mapema ili kuepuka kuvamiwa na kuporwa fedha za mauzo wakielekea kwenye makazi yao.

**Mwenyekiti wa wafanyabishara wa kata hiyo, Magembe Chimu alisema kila mwananchi ameshiriki kujitoa katika michango na kukodisha nyumba hiyo...**

Mwenyekiti wa wafanyabishara wa kata hiyo, Magembe Chimu alisema kila mwananchi ameshiriki kujitoa katika michango na kukodisha nyumba hiyo na kulipia kodi ya mwaka mmoja.

Alisema, kumekuwepo na uvamizi wa wizi kwenye makazi yao, vibanda vya biashara pamoja na kinadada kunyang'anywa mikoba na simu, vitendo vinavyofanywa nyakati za usiku. Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mhongolo, Anitha Ngeiyamu alisema wazo la kuanzisha kituo hicho lilianza baada ya wananchi na wafanyabiashara kuingiwa hofu juu ya kukithiri kwa uhalifu huo, hivyo kulishirikisha Jeshi la Polisi Mkoa ambalo liliridhia juu ya uamuzi huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi akizindua na kukipokea kituo hicho, alisema hatua hiyo inafaa kuigwa na wananchi wa kata nyingine, ili kusogeza huduma karibu na wananchi kwani serikali haiwezi kufanya kila kitu peke yake na kuahidi kupeleka polisi na kukabiliana na wimbi hilo la uhalifu uliopo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA)Mhandisi Yusuph Katopola (kulia) akikagua upanuzi wa mtambo wa kuchakata tope kinyesi kutoka kuchakata lita za ujazo 40 kwa siku hadi kufikia 100 ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Shinyanga, juzi, **PICHA: MARCO MADUHU**

# Dk. Biteko awaita wawekezaji Kagera

**Na Restuta Damian,** KAGERA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk.Dotto Biteko amewataka wawekezaji kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Kagera kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizopo mkoani humo ili kuendelea kuinua uchumi wa mkoa huo.

Dk.Biteko alibaini hayo juzi katika Jukwaa la Uwekezaji mkoani hapa ikiwa ni mwendelezo wa wiki ya tamasha la Ijuka Omuka linalolenga kuwahimiza wazawa wa Mkoa huo, kurudi , kuwekeza nyumbani na kuchochea uchumi wa mkoa huo na kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

"Najua kuna wawekezaji wengi wanataka kuja lakini maneno ya kukatisha tamaa huwa hayaishi na vikwazo mbalimbali, kama tutaondoa vikwazo na kuwaunga mkono Mkoa wa Kagera utabadilika," alisema Dk. Biteko

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwasa alisema wawekezaji ni wakati wao sasa kuja kuwekeza mkoani hapa kwani jiografia na mwingiliano wa watu ni mkubwa kutokana na kupakana na nchi zenye idadi kubwa ya watu wanaojihusisha na biashara mbalimbali.

Alisema pamoja na mambo mengine, mkoa huu umejaliwa rasilimali mbalimbali za uwekezaji ikiwemo uvuvi lakini imekuwa ni sehemu kubwa ya upotevu wa mapato kutokana na kutokuwa na uwekezaji wa kutosha.

Alisema matamanio yake ni kuona wanaanzisha ufugaji wa vizimba vya dagaa na samaki, kuwekeza kwenye kukausha dagaa pamoja na uhifadhi rafiki wa mazao hayo ambayo soko lake kubwa lipo nchini Rwanda.

Mhandisi Emmanuel Manyanda kutoka Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) alisema usanifu wa miradi ya kimkakati ya stendi, kingo za Mto Kanoni pamoja na soko la kisasa umekamilika na kuwa utekelezaji wa miundombinu hiyo utaleta unafuu na fursa katika shughuli za uwekezaji.

Baadhi ya wananchi mkoani hapa akiwemo Jamshid Jamal mkazi wa Kata ya Miembeni, aliambia Nipashe kwamba mkoa huo una fursa nyingi za kilimo, uvuvi na ufugaji.

Alisema hata hali ya hewa ni nzuri lakini bado elimu ya uwekezaji haijatolewa vya kutosha ili kuusaidia kusonga mbele zaidi.

# TCRA yaonya maudhui yasiyofaa mitandaoni

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kanda ya Ziwa imewataka wamiliki pamoja na waendeshaji wa vyombo vya habari vya mitandaoni kuzingatia sheria katika uchapishaji maudhui.

Pia, wametakiwa kuepuka maudhui yasiyofaa na yanayoenda kinyume cha sheria.

Hayo yamebainishwa juzi wilayani Musoma na Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) Kanda ya Ziwa, mhandisi Imelda Salum katika semina na waandishi wa habari kutoka Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mara (MRPC).

Mhandisi Imelda alisema baada ya mamlaka hiyo kubaini kuwepo kwa maudhui zisizofaa mitandaoni imeona ni vyema kufanya semina na wadau hao na kuwapa uelewa hususani katika eneo la maudhui mtandaoni.

"Kwa vile vyombo vingi vinapeleka maudhui huko na tunatarajia baada ya mafunzo haya watachukua hatua stahiki sambamba na kuomba leseni," alisema Imelda.

Aidha, aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari mkoani hapa kurasimisha vyombo na kazi zao kwa kuomba leseni ili waweze kuendesha shughuli zao kwa kutambulika.

Mhandisi wa mamlaka hiyo, Aude Kileo alisema mfumo wa utoaji leseni ulianzishwa Februari 23, 2005 na kuingizwa kwenye Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Namba 3 ya Mwaka 2010 (EPOCA)

"Mwenye leseni kama atahitaji kuendelea kutoa huduma za mawasiliano atatuma maombi kabla ya leseni kuisha muda wake, muda wa kutuma maombi ni miezi miwili kwa leseni ndogo, kwa leseni kubwa ni miezi 12 kabla ya muda wake kuisha," alisema.

Mwenyekiti wa MRPC, Jacob Mgini alisema ni vyema wana habari hasa wa mitandaoni kuendelea kufuata sheria na kanuni pamoja na misingi ya taaluma hiyo katika utendaji kazi wao.

Asha Shabani ni miongoni mwa waandishi walioshiriki katika semina hiyo alisema mafunzo hayo yatawasaidia kwa sababu vyombo vya habari kadhaa vimekuwa vikikumbwa na kesi mbalimbali kwa kutokujua kanuni za sheria.

Nipashe
Spotika



WANASOKA BORA 15 WA KIAFRIKA WA WAKATI WOTE UK. 12



Mshindi wa Tuzo ya Mchezaji Bora wa Fifa wa Mwaka 2024, Vinicius Junior (kushoto), akipongezwa na rais wa Shirikisho hilo la Soka duniani, Gianni Infantino, Desemba 17, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# KURA ZA KUSHANGAZA TUZO YA MCHEZAJI BORA WA FIFA

**PARIS, Ufaransa**

HUENDA ikakosa uzuri na hadhi ya Ballon d'Or, lakini tuzo ya FIFA ya mwanasoka bora wa mwaka bado inapamba vichwa vya habari kila mwaka.

Hafla hiyo ilifanyika Jumanne ya Desemba 18 ambapo manahodha na makocha wa timu za taifa ndio wapigaji wa kura, huku Vinicius Junior akiitwaa baada ya kuikosa ile ya Ballon d'Or.

Raia huyo wa Brazil aliwashinda bingwa wa Ballon d'Or, Rodri pamoja na Jude Bellingham, Dani Carvajal, Lamine Yamal na wengine.

Ilikuwa tuzo yake ya kwanza kwa winga huyo wa Real Madrid, ambaye alipigiwa kura na mchanganyiko wa manahodha na makocha wa timu za taifa, waandishi wa habari na mashabiki.

Wakati Vinicius alikuwa mshindi aliyestahili wa Tuzo Kuu ya FIFA katika soka la wanaume, kulikuwa na kura ambazo ziliibua mshangao.

**Harry Kane amkataa Bellingham**

Upigaji kura wa tuzo za soka mara nyingi huwaona wachezaji wenzao wakishikamana na kusaidiana. Lakini nahodha wa Timu ya Taifa ya England na fowadi wa Bayern Munich, Harry Kane, aliamua kutomtunuku Muingereza mwenzake, Bellingham katika kura yake.

Kane alimweka Bellingham katika nafasi ya pili, huku Rodri akishika nafasi ya kwanza na mshindi Vinicius akishika nafasi ya tatu.

Bellingham aliingia kwenye tuzo hizo baada ya mwaka wa kustaajabisha na Real Madrid. Alishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na 'Los Blancos' hao, huku pia akiisaidia England kufika fainali ya Euro 2024.

**Vyombo vya habari vya Argentina vyampuuza Messi**

Lionel Messi hatakiwi kufanya mambo mengi sana ili aonekane kwenye orodha fupi ya tuzo kuu za soka siku hizi. Messi tayari ameshinda mara nane tuzo ya Ballon d'Or, alishinda Copa America 2024, lakini bila shaka hakuwa miongoni mwa wanasoka 11 bora zaidi wa kiume duniani mwaka huu.

Mwandishi wa habari wa Argentina, Claudio Mauri yeye hakumpigia kura Messi, badala yake alimchagua Rodri, Lamine Yamal na Toni Kroos.

Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni, alimpigia kura Messi, na kumweka katika nafasi ya kwanza. Messi mwenyewe alimpigia kura Yamal.

**Erling Haaland akataliwa Norway**

Jina la Erling Haaland lilikuwa moja wapo ya chaguo maarufu zaidi kati ya wapigakura, akimaliza katika nafasi ya nane.

Fowadi huyo wa Manchester City alishinda Ligi Kuu England na kumaliza kama mfungaji bora msimu wa 2023/24, lakini alizidiwa na mwenzake Rodri.

Ni wazi nahodha wa Norway na Arsenal, Martin Odegaard alihisi vivyo hivyo. Alimweka mchezaji mwenzake wa kimataifa katika nafasi ya tatu, akiwaweka Rodri na Vinicius mbele yake, huku kocha wa Norway, Stale Solbakken akimweka Haaland nafasi ya pili.

Haaland pia alinyimwa nafasi ya kwanza na mwakilishi wa vyombo vya habari vya Norway, Morten Pedersen, ambaye, kama Odegaard, alimchagua katika nafasi ya tatu.

**Makocha wa timu za taifa**

Makocha wa timu za taifa hutazama soka kwa miezi michache tu ya mwaka kulingana na upigaji kura. Mabosi wengi wa timu ya taifa walipanga viwango vitatu vya juu vya ajabu, zaidi ya kocha wa Uswisi, Murat Yakin.

Wachezaji watatu bora kati ya Florian Wirtz (wa kwanza), Federico Valverde (wa pili) na Lamine Yamal (wa tatu) watawashangaza wachache, huku Rodri na Vinicius wote wakipuuzwa.

Kocha wa Ujerumani, Julian Nagelsmann bila mshangao aliwateua Wajerumani Wirtz na Toni Kroos, akiwaacha Vinicius, huku Kocha wa Ubelgiji, Domenico Tedesco akiwateua Yamal, Wirtz na Haaland kama watatu anaowapendelea zaidi.

## ISIKUPITE

BUKAYO Saka (23), ambaye ana mabao 52 na asisti 44 tangu 2019, kabla ya kuumia juzi kwenye mechi dhidi ya Crystal Palace, alicheza mechi yake ya 250 na Arsenal, na kumfanya kuwa Mwingereza mwenye umri mdogo zaidi kufanya hivyo kwa klabu hiyo.



Extra Time

# WANASOKA BORA 15 WA KIAFRIKA WA WAKATI WOTE


SALAH

**LONDON, England**

KWA muda mrefu Afrika imetoa baadhi ya nyota wa muda wote wa soka, ambao wengi wao wametamba na vipaji vyao barani Ulaya.

Nyota kutoka Cameroon, Nigeria na Misri, wamevutia watazamaji kote ulimwenguni, wakiandika majina yao katikati vitabu vya historia ya soka.

Wengi wa wanasoka wenye furaha barani Afrika wametundika daruga zao katika karne ya 21, lakini bado kuna idadi kubwa ya nyota ambao wanang'ara katika kiwango cha juu.

Hawa ndio wanasoka bora zaidi wa Kiafrika wa wakati wote;

**15. Lauren Mayer**

Lauren alikuwa mmoja wa wengi walioelewa na Arsene Wenger na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Cameroon alimzawadia kocha wake kwa kiwango bora kabisa. Alipowasili mwaka 2000 pale Arsenal, Lauren alikuwa muhimu kwa ushindi wote wa Arsenal wa karne ya 21 wa Ligi Kuu England, ikiwa ni pamoja na kupanga safu ya beki wa kulia wakati wa kampeni ushindi wa taji la ligi bila kupoteza.

Mshindi wa Kombe la FA akiwa na Portsmouth na bingwa mara mbili wa Kombe la Mataifa ya Afrika akiwa na Cameroon, Lauren alistaafu soka ya kimataifa akiwa na umri wa miaka 25 pekee.

**14. Thomas N'Kono**

Wachezaji wakuu wa Afrika mara nyingi wamekuwa wakitamba kwenye uchezaji wa ndani, lakini Thomas N'Kono alikuwa golikipa. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Cameroon mwenye michezo 63 aliiwakilisha nchi yake kwa miongo miwili na mara nyingi alikuwa na uchezaji wa kuvutia macho katika mashindano makubwa.

Akiwa kwenye michuano ya Kombe la Dunia la FIFA mara tatu, alibeba mara mbili tuzo ya Mwanasoka Bora wa Afrika na alitamba sana kwenye Kombe la Dunia la 1990 huku Cameroon ikifika hatua ya robo fainali.

**13. Jay-Jay Okocha**

Jay-Jay Okocha alifanya mamilioni ya Wanigeria kupenda soka. Akiwa maarufu kwa ustadi wake wa chenga za maudhi, nyota huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain na Bolton Wanderers, alicheza kwa furaha kubwa iliyowaacha watazamaji wakishangilia.

**12. Pierre-Emerick Aubameyang**

Pierre-Emerick Aubameyang amefifia hadi kusikojulikana kidogo katika zama za kisasa, sasa anacheza kwenye Ligi Kuu ya Saudi Arabia. Si rahisi kusahau jinsi mchezaji huyo wa Kimataifa wa Gabon alivyokuwa bora wakati wa miaka yake ya kilele akiwa Borussia Dortmund na Arsenal.

**11. Nwankwo Kanu**

Akiwa ameshindwa kukidhi mahitaji ya Inter Milan baada ya kuibukia Ajax, Wenger alimchukua Nwankwo Kanu pale Arsenal. Imani ya kocha huyo wa Ufaransa ilizaa matunda haraka huku Mnigeria huyo akichanua na kuwa bora kule Kaskazini mwa London.

Kanu alikuwa akivutia mara kwa mara kwani 'Washikabunduki' walishinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya England, hata kama hakuwahi kuwa nyota wa mchezo kule Highbury.

**10. Roger Milla**

Roger Milla mfungaji mwenye umri mkubwa zaidi katika historia ya Kombe la Dunia (miaka 42 na 39) aliifungia Cameroon mabao manne kwenye Kombe la Dunia la 1990.

Maisha marefu ya Milla yalikuwa ya kuvutia kama vile mabao yake yanavyorejea kwa nchi yake, huku fowadi huyo akitumia muda mwingi wa maisha yake ya klabu kama mshambuliaji wa kutegemewa nchini Ufaransa.

**9. Michael Essien**

Michael Essien katika kilele chake alikuwa kiungo mkabaji mgumu, anayecheza mpira kwa kasi na raia huyo wa Ghana alifanikiwa kuichezea Chelsea kwa kipindi cha miaka tisa.

Bingwa huyo mara mbili wa Ligi Kuu England, mshindi mara nne wa Kombe la FA na mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msmu wa 2011/12, alionesha mabadiliko katika safu ya kiungo ya 'The Blues' walipochanua na kuwa nguvu kubwa duniani.

**8. Riyad Mahrez**

Leicester City walimsajili Riyad Mahrez kwa pauni 450,000 kutoka Le Havre mwaka 2014. Ingawa raia huyo wa Algeria alicheza vizuri katika miezi 18 ya kwanza pale kwenye Uwanja wa King Power ni msimu wa 2015/16 ambao ulimfanya ajijengee sifa kubwa zaidi.

Mshiriki muhimu wa kikosi cha Leicester kilichoshinda taji la Ligi Kuu England, winga huyo alikuwa mtoa huduma wa mara kwa mara wa Jamie Vardy na mfungaji mabao na hatimaye Manchester City wakamsajili mwaka 2018.

**7. Abedi Pele**

Abedi Pele hakulazimika kungoja mashindano ya kimataifa ili aonekane kwa watazamaji wa Ulaya. Raia huyo wa Ghana alijiunga na Marseille mwaka 1987 na kujitangaza kwa haraka kama mmoja wa vipaji vya ajabu sana kutoka barani Afrika.

Akiwa sehemu ya washambuliaji watatu mashuhuri wa Marseille pamoja na Chris Waddle na mshindi wa Ballon d'Or, Jean-Pierre Papin, Pele alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 1992/93.

**6. Sadio Mane**

Sadio Mane alitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England akiwa na Liverpool baada ya kusajiliwa kutoka Southampton mwaka 2014. Alifunga mabao 21 katika misimu miwili ya ligi akiwa na Saints hao.

Liverpool walitumia fedha nyingi kumnunua nyota huyo wa Senegal huku kocha Jurgen Klopp akianza mapinduzi yake pale Anfield na Mane akaonekana kuwa sehemu muhimu. Winga huyo asiyechoka dimbani alikuwa mfungaji mabao aliyebobea, mpiga chenga mwenye nguvu na mchezaji wa kuvutia, akiunda safu ya wachezaji watatu wanaoheshimika zaidi enzi hizi pamoja na Roberto Firmino na Mohamed Salah.

Alishinda Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumaliza wa pili katika kura ya Ballon d'Or mwaka 2022.

**5. Yaya Toure**

Msimu wa 2013/14, Yaya Toure alikuwa kitu kingine. Wakati Manchester City ikipambana na Liverpool ikielekea kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast, ndiye aliyekuwa akivuta kamba na kuamua mechi.

Mabao 20 kwenye Ligi Kuu kutoka kwa kiungo wa kati si jambo la kawaida.

Toure alitwaa tuzo ya Mwanasoka Bora wa Afrika wa Mwaka mara nne.

**4. George Weah**

Mwafrika pekee aliyeshinda Ballon d'Or - ukiondoa Eusebio mzaliwa wa Msumbiji ambaye aliichezea Ureno - George Weah alikuwa mtu wa kuvutia katika miaka ya 1990. Akibeba tuzo ya hadhi ya juu zaidi ya soka mwaka 1995 akiwa anaichezea AC Milan

Raia huyo wa Liberia alishinda mataji mawili ya Serie A nchini Italia akiwa tayari amefanya vema nchini Ufaransa.

**3. Didier Drogba**

Iwapo uliwahi kuhitaji mchezaji ili kutoa wakati wa uhakika katika uangalizi mkali zaidi, Didier Drogba, ndiye aliyekuwa mtu wa kumpigia simu. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast alikuwa mwanga mkali katika kikosi cha Chelsea kilichovutia wakati wa mastaa na mwanzoni mwa miaka ya 2010, akiongoza mstari kwa mchanganyiko kamili wa nguvu na usahihi.

Drogba alifunga mabao tisa katika fainali kumi alipokuwa akiichezea 'The Blues', likiwamo bao la kusawazisha na penalti ya ushindi huku Chelsea ikishinda taji lao la kwanza kabisa la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2011/12.

Mataji manne ya Ligi Kuu na mengi zaidi ya Kombe la FA yanapatikana kwenye kabati la kuvutia la mshambuliaji huyo, huku Drogba akipewa heshima kubwa na mashabiki wa Chelsea katika kipindi cha mafanikio zaidi ya klabu hiyo.

**2. Samuel Eto'o**

Samuel Eto'o alichukua njia ya ajabu kidogo hadi kwenye ustaa mkubwa. Baada ya kusajiliwa na Real Madrid mwaka 1997, raia huyo wa Cameroon alicheza kwa mkopo katika klabu kadhaa za Hispania kabla ya kuwasha moto huko Mallorca.

Barcelona ndiko sehemu alikotamba zaidi Eto'o ambako alitwaa mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na matatu ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Kuhamia Inter kulizaa mafanikio zaidi na taji lingine la Ligi ya Mabingwa, huku pia akitwaa tuzo ya Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Afrika mara nne.

**1. Mohamed Salah**

Sasa tunakuja kwa mkuu zaidi, Mohamed Salah.

Ingawa mabishano yanaweza kutolewa kwa mastaa kama Weah, Drogba na Eto'o. Salah ndiye kinara kwa ubora.

Baada ya kushindwa kufanya vizuri Chelsea, Salah alijenga upya heshima yake nchini Italia akiwa na Fiorentina na AS Roma, na kuwashawishi Liverpool kumsajili mfalme huyo wa Misri.

Bado anaendelea kucheza na bila shaka yoyote bado ana mengi mazuri ya kufanya.

## Nukuu

"Alihisi kitu kwenye misuli yake ya paja, hakuweza kuendelea, itabidi atathminiwe. [Nina] wasiwasi sana kuhusu huyo. Ni vigumu kujua atarejea lini, wamempima lakini ni vigumu sana kusema ni mbaya kiasi gani," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akizungumzia majeraha ya Bukayo Saka baada ya kuumia dakika ya 24 ya mchezo wakati wakishinda mabao 5-1 dhidi ya Crystal Palace juzi.**



"Ubora tuliocheza, jinsi tulivyocheza ... nadhani kila mtu hapa chumbani anaweza kuona hii. Hii pia ni mtindo jinsi Barca wanataka kucheza, jinsi wanavyotaka kutawala, lakini mwisho ni mpira na timu ambayo inafunga mabao mengi zaidi, sote tumesikitishwa na kushindwa huku kwa sababu tulicheza kwa ustadi. Sasa tutasherehekea Krismasi, tutaanza mazoezi Desemba 29 na kuzingatia kile tunachoweza kufanya katika nusu ijayo ya msimu," **Kocha wa Barcelona, Hansi Flick, baada ya kipigo cha mabao 2-1 kwenye LaLiga juzi, kutoka kwa Atletico Madrid.**



"Suluhu ni kuwarudisha wachezaji. Tuna beki mmoja wa kati aliye fiti, hiyo ni ngumu. Tutaenda kujaribu mchezo ujao. Kwa kweli kuna sababu zaidi, tunaruhusu mabao ambayo hatukuruhusu zamani, [hatufungi] mabao tuliyofunga hapo awali. Soka si sababu moja tu, kuna sababu nyingi ndogo, msimu uliopita tulitwaa ubingwa wa Ligi Kuu, lakini tulikuja hapa na kushindwa," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baada ya kipigo cha mabao 2-1 nyumbani kwa Aston Villa, juzi.**



Nipashe
Spotika

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 23, 2024

# MABEKI WAKALI WA NYAVU LIGI KUU TANZANIA BARA

**Na Adam Fungamwango**

JUKUMU mama la kwanza kwa mabeki, siku zote ni kuzuia mashambulizi kutoka timu pinzani, lakini kwa soka la kisasa, wanawajibika pia katika kufunga, hivyo kuna mabeki ambao wamejaliwa vipaji au kuwa na uwezo wa ziada wa kusaidia mashambulizi na kufunga mabao.

Kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea kuna mabeki ambao wamefunga na kuzisaidia timu zao kupata ushindi au kuziongezea idadi ya mabao.

Mpaka sasa wapo mabeki ambao wana mabao zaidi ya moja hadi kufikia mechi za mzunguko wa kwanza, huku baadhi ya timu zikiwa bado hazijamaliza.

Katika makala haya, tunakuletea mabeki ambao wamefunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa...

**1# Shomari Kapombe (Simba)**

Ni beki wa kulia wa Simba ambaye kwa sasa ana mabao mawili mpaka sasa. Juzi alifunga bao kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 5-2. Aliunganisha mpira wa krosi kutoka kwa Mohamed Hussein 'Tshabalala.'

Awali, mchezaji huyo alifunga bao lake la kwanza Oktoba 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Simba ikicheza dhidi ya Namungo na kushinda mabao 3-0.

**2# Ibrahim Hamad 'Bacca' (Yanga)**

Beki huyu wa kati wa Yanga, amefunga mabao mawili mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Yote ameyaweka wavuni kwa kichwa.

Bao lake la kwanza alilifunga Septemba 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya, likiwa bao pekee ambalo Yanga iliifunga KenGold.

Oktoba 3, mwaka huu, 'Bacca', alifunga bao lingine kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Yanga ikiifunga Pamba Jiji mabao 4-0.




Beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, akishangilia bao alilofunga juzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uliochezwa Uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera, kati ya timu hiyo na Kagera Sugar, akiiwezesha kushinda mabao 5-2. **MPIGAPICHA WETU**

**3# Antony Trabita (Singida)**

Huyu ni beki wa kati wa Singida Black Stars raia wa Ivory Coast, naye ana mabao mawili mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alifunga bao Agosti 23, mwaka huu, likiiwezesha timu yake kushinda bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Novemba 25, mwaka huu, alifunga bao lingine kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Singida Black Stars ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tabora United.

**4# Fondoh Che Malone (Simba)**

Che Malone ni beki wa kati wa Simba, raia wa Cameroon ambaye msimu huu ameonekana kuwa kwenye kiwango bora na mpaka sasa akiwa na mabao mawili.

Bao la kwanza alilifunga Agosti 17 mwaka huu, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, wakati Simba ikiizamisha Tabora United mabao 3-0.

Lingine alilifunga Oktoba 22 kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya, alipofunga bao pekee timu yake ikishinda 1-0 dhidi ya Prisons.

**5# Erasto Nyoni (Namungo)**

Beki wa kati mkongwe nchini, Erasto Nyoni, ameweka rekodi ya kufunga mabao mawili kwa mchezo mmoja.

Ilikuwa ni Desemba 15, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, alipofunga mabao mawili kwenye mchezo dhidi ya KenGold, akiiwezesha Namungo kushinda mabao 3-2 dhidi ya wenyeji wa mchezo huo.

**6# Nicolaus Gyan (Fountain Gate)**

Raia huyu wa Ghana ambaye alipoingia nchini kuichezea Simba alikuwa anacheza kama straika, lakini baadaye akabadilika na kuwa beki wa kulia. Mpaka sasa ameendelea kucheza kwenye nafasi hiyo na amekuwa moja ya mabeki mwenye uwezo wa kufunga mabao.

Oktoba 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Tanzania Kwaraa, Manyara alifunga bao moja, akiwezesha timu yake ya Fountain Gate kutoka sare ya mabao 2-2, Desemba 13 mwaka huu, kwenye uwanja huo huo alifunga bao katika mchezo ambao timu yake ilishinda mabao 3-2.

**JE, WAJUA?**



USHINDI wa mabao 2-1 iliyoupata Atletico Madrid katika Uwanja wa Estadi Olimpic Lluis dhidi ya Barcelona, unamaanisha sasa Atletico itamaliza mwaka 2024 ikiwa kileleni mwa msimamo wa LaLiga baada ya kukusanya alama 41, ikifuatiwa na Barca (pointi 38) na Real Madrid (pointi 37). Hata hivyo, Barca imecheza mechi 19, Atletico (18) na Madrid (17).



# 27 wapatiwa matibabu kambi ya madaktari bingwa Kondoa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MADAKTARI bingwa kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH) wamefanikiwa kuwafanyia upasuaji wagonjwa 27 waliokuwa wakisumbuliwa na magonjwa mbalimbali.

Upasuaji huo ulifanyika wilayani Kondoa mkoani hapa katika kambi ya siku nne. Kambi hiyo ilizinduliwa rasmi wilayani humo na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Ashatu Kijaji, ikijumuisha madaktari bingwa wa magonjwa mbalimbali. Akizungumza baada ya kuhitimishwa kambi hiyo, Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama na afya ya uzazi, Ezrael Soko alisema wagonjwa hao walipatiwa huduma mbalimbali ikiwemo upasuaji kwa kutumia magari maalumu ya kutoa huduma za kibingwa.

Alisema wametoa matibabu ya kibingwa ya upasuaji wa jumla katika magonjwa mbalimbali ikiwemo macho, magonjwa ya kinamama na afya ya uzazi, mifupa pamoja na magonjwa mengine.

"Mwitikio wa wagonjwa waliojitokeza kufanyiwa uchunguzi ikiwemo kupatiwa matibabu ulikuwa mkubwa, tunaishukuru serikali kuwekeza kwenye sekta ya afya na kupelekea huduma hizi kufanyika,"alisema Dk. Soko Alisema, BMH inaendelea kutoa huduma za kibingwa katika maeneo ya mbali na huduma ikiwemo kuwajengea uwezo wataalamu ngazi za wilaya na mikoa katika kutekeleza maelekezo ya serikali kupitia Wizara ya Afya ya kutoa huduma za afya kupitia kliniki tembezi.

**"Mwitikio wa wagonjwa waliojitokeza kufanyiwa uchunguzi ikiwemo kupatiwa matibabu ulikuwa mkubwa, tunaishukuru serikali kuwekeza kwenye sekta ya afya..."**

"BMH inaendelea kutoa huduma za kibingwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo kuwajengea uwezo wataalamu ngazi za wilaya na mkoa ili kuendelea kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa,"alisema Dk. Soko.

Alisema kambi hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wilayani Kondoa, ambapo kuwasogezea huduma za kitabibu wagonjwa hao kumewapunguzia gharama ya kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kufuata huduma.

Habibu Issa mkazi wa kijiji cha Hamai wilayani Kondoa alisema kambi hiyo imekuwa msaada mkubwa sana kwa wakazi wa wilaya hiyo kwa sababu imewasaidia kupunguza gharama za kusafiri kwenda nje ya wilaya hiyo kupata matibabu ya kibingwa.

Alisema wanawashukuru madaktari bingwa kutoka BMH pamoja na wataalamu wa afya kutokana na huduma bora ambazo waliwapatia wagonjwa waliojitokeza katika hospitali ya Bukulu iliyopo Halmashauri ya Kondoa.

Pia, aliishukuru serikali kufanya uwekezaji katika sekta ya afya na kupelekea huduma za kibingwa kufanyika katika maeneo mbalimbali hapa nchini kumesaidia kuokoa maisha ya wananchi mbalimbali.



Baadhi ya watumishi wa moja ya kampuni inayoshughulikia upimaji wa ardhi na shughuli za kijamii mkoani Dodoma .wakiwahudumia kwa kuwalisha chakula wazee wasiojiweza wanaoishi kituo cha Mother Tereza kilichopo Hombolo Bwawani Jiji la Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Walimu wakoshwa uanzishaji kliniki kusikiliza kero zao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADHI ya walimu jijini Dodoma wameipongeza serikali kwa kuanzisha kliniki maalumu ya kushughulikia kero zinazowasibu walimu nchini, ikiwemo malipo ya malimbikizo ya madeni ya mishahara mipya na likizo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jijini hapa jana kuhusu kliniki hiyo maalumu walisema kuwa itasaidia kutatua kero ambazo zimewakabili kwa kipindi kirefu.

Mmoja wa walimu hao, Prisca Barnabas alisema wanaiomba serikali kuharakisha kuwafikishia huduma hiyo ndani ya mkoa wao kwani dhumuni la Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona walimu wakiwa kwenye mazingira mazuri ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Aidha, alisema walimu hivi sasa bado wanakabiliwa na changamoto nyingi ambazo kliniki hiyo inaweza kuwa dawa ya kuzitibu.

"Walimu bado tunachangamoto nyingi ikiwemo upandaji wa madaraja, mishahara, likizo, malimbikizo ya madai yetu ambayo kupitia kliniki hii tunaweza kwenda kuzimaliza"alisema

Kadhalika alisema wanaupongeza uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa jitihada za kushugulikia kero za walimu kwa kushirikiana na serikali.

"Tunamshukuru sana Rais Samia kwa kliniki hii lakini pia viongozi wetu wa CWT, Rais pamoja na Katibu Mkuu wetu Joseph Misalaba kwa namna ambavyo wamekituliza chama na nitoe wito kwa walimu wenzangu kutumia fursa hii kutatua kero zao za muda mrefu"alisema

Mwalimu Ahemed Ng'eni, alisema kliniki hiyo itasaidia walimu ambao wamekuwa hawana uwezo wa kufika katika makao makuu ya wilaya ili kupata huduma wanazozihitaji.

"Nipongeze sana serikali yetu kuanzisha kliniki hii kwani inakwenda kuwa msaada kwa walimu katika maeneo yote ya nchi kwakuwa itakwenda kuanzia ngazi ya kata hadi taifa hivyo tutapata fursa ya kutatuliwa kero zetu za muda mrefu na kuongeza ufanisi kazini" alisema

Kliniki ya kushugulikia kero za walimu ni agizo lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kusiliza kero zao na kuzifanyia kazi kuanzia ngazi ya kata hadi taifa.

# H'shauri ya Ikungi yatoa mil.278/- kwa vikundi 17

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida imekabidhi hundi ya Sh. milioni 278.2 kwa vikundi 17, ikiwa ni mkopo wa asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Ally Mwanga, alikabidhi hundi hizo juzi na kutoa onyo kwa vikundi vitakavyokwenda kinyume na makubaliano yaliyowekwa katika mikopo hiyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Mwanga ambaye alimwakilisha Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu, alisema kumeibuka tabia ya vikundi kubadili matumizi ya fedha za mikopo na wengine kukimbia na fedha hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema wameshatoa mikopo ya Sh. milioni 852.1 kwa vikundi 271 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hadi sasa.

Alitoa mchanganuo kuwa katika vikundi 271 vya wanawake vilikuwa ni 186 ambavyo vilipewa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 476.9, vikundi vya vijana 58 mikopo ya Sh.milioni 303.2 na vikundi vya watu wenye ulemavu 27 mikopo ya Sh. milioni 71.9.

"Katila vikundi hivyo wanufaika 1,870 walipata mikopo hiyo iliyowawezesha kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi, ufugaji , kilimo, biashara ndogondogo na Tehama," alisema.

Kijazi alisema changamoto zilizopo katika utoaji wa mikopo ya halmashauri ni baadhi ya vikundi kutorejesha mikopo kwa wakati, vikundi kubadili matumizi ya fedha walizokopeshwa hata kabla ya kutekeleza miradi waliyoombea fedha.

Changamoto nyingine ni mabadiliko ya hali ya hewa kuathiri miradi ya kilimo, uhaba wa bei kubwa kwa baadhi ya malighafi za miradi, hivyo kukwamisha uendelevu wa miradi.

Nyingine ni kukosekana kwa mtandao wa usajili kwenye baadhi ya maeneo, uhaba wa vitendea kazi kwa wataalamu wanaoratibu mikopo.

"Kwa niaba ya wananchi wa Ikungi naishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa mikopo hii kwa wananchi na kuridhia ianze kutolewa tena baada ya kuboreshwa taratibu za utoaji na usimamizi wa mikopo," alisema.

Baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo waliishukuru serikali kwa kushirikiana vyema na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kurejesha mikopo hiyo wakisema imekuwa msaada kuwainua kiuchumi hususani wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalumu.





# Kigogo CCM ataja mbinu kukabili uhaba wataalamu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JAMII imetakiwa kuweka jitihada kwenye kusomesha watoto ili wapate elimu itakayosaidia kukabiliana na uhaba wa wataalamu wenye ujuzi mbalimbali katika maeneo yao.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Mlezi wa mkoa wa Njombe, Halima Mamuya katika mkutano wa kuwasilisha utekelezaji wa Ilani ya CCM katika kipindi cha Julai 2020 hadi Desemba 2024 katika jimbo la Njombe mjini.

Alisema serikali imefanya kazi kubwa katika kufungua sekta za elimu, afya, kilimo, ufugaji, huduma za maji, umeme na madini hivyo ipo haja jamii kuunga mkono kwa kuwaandaa watoto.

"Sasa kazi yenu ni kufanya maandalizi ya wataalamu katika sekta zote ambazo zimefunguliwa, katika sekta zote ambazo zimeendelezwa na nisingependa siku moja nifike Makete alafu waniambie walimu hawatoshi angalieni watoshe tena wawe wenu wenyewe," alisema Halima.

Alisema wakati serikali inaendelea kuboresha nyanja mbalimbali, jamii haipaswi kuwa nyuma badala yake ijiwekee mikakati ya kuhakikisha inaungana na serikali katika fursa hizo.

"Wakati haya mengine yote yanafanyika na nyinyi mfanye yenu, imeguswa hapa sekta ya kilimo wanataka maofisa ugani lakini lazima mfike mahali mseme kwamba sisi wenyewe tunao, isingekuwa vema sekta ya madini imefunguliwa halafu nyinyi hamna wataalamu," alisema Mamuya.

**"Sasa kazi yenu ni kufanya maandalizi ya wataalamu katika sekta zote ambazo zimefunguliwa, katika sekta zote ambazo zimeendelezwa na nisingependa siku moja nifike Makete alafu waniambie walimu ...**

Hata hivyo Halima alimpongeza mbunge huyo kwa kutekeleza vizuri ilani ya CCM kwa kuhakikisha anawaletea maendeleo wananchi.

Awali, Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika alisema katika jimbo hilo mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 300 imesainiwa na kampuni tofauti kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta za kilimo, maji, barabara, elimu na afya.

"Njombe tuna miradi mikubwa miwili ya kimkoa, tuna mradi wa shule ya wasichana ya kisasa huko Wanging'ombe na ndani ya mji wa Njombe tuna mradi mkubwa wa kitaifa wa chuo kikuu ambao ni shilingi bilioni 18 na umeanza hatua za awali za utekelezaji na fedha zake zimetengwa," alisema Mwanyika.

Alisema wakati anaomba kura za ubunge kulikuwa na tatizo kubwa la mgawo wa maji, barabara mbovu katikati ya mji na zinazoelekea maeneo ya uwekezaji, uhaba wa walimu na vyumba vya madarasa lakini zinakwenda kuwa historia.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Njombe, Jastin Nusulupila alitoa rai kwa wanachama wa chama hicho kwenda kuwaambia wananchi kazi zote ambazo zimefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wao wajumbe akiwemo Christina Ramso alisema kuna hatua imepigwa katika huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali na kumuomba mbunge huyo kuendelea kuwaletea maendeleo katika jimbo hilo.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Khamis akiagana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, baada ya kumaliza kufungua mafunzo ya Usambazaji na Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa viongozi na watendaji wa halmashauri ya wilaya ya Mbeya vijijini, yaliyofanyika katika ukumbi wa shule ya sekondari Mbalizi Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati: Wakulima kupewa zana za kisasa za kilimo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Deo Mwanyika amesema serikali imepanga kuwawezesha wakulima zana za kisasa za kilimo ikiwemo matrekta ili waweze kufanya uzalishaji wenye tija.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati kamati hiyo ilipotembelea vituo vya rasilimali za kilimo katika Halmashauri ya Mji wa Njombe na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mwanyika alisema vituo hivyo vinapaswa kufanya kazi kisasa na kuachana na zana za zamani ambazo zimepitwa na wakati.

"Lazima twende mahali pakubwa zaidi kwa sababu vituo hivi vimetoa mafunzo ambayo wananchi wanaendelea kuyatumia, hivi vituo vimeleta manufaa makubwa tunataka kutanua kwa kuleta zana za kisasa zaidi," alisema Mwanyika. Mwanyika alisema serikali inatambua mchango wa sekta ya kilimo kwa pato la taifa na kwamba mbali na ruzuku kwenye mbolea na viuatilifu hivi sasa inatoa zana za kisasa ikiwemo matrekta ili wakulima wapate fursa ya kukodishwa kwa gharama nafuu.

Aidha kamati hiyo iliagiza kufanyika kwa maandalizi ikiwemo ujenzi wa uzio katika vituo hivyo ili serikali iweze kuja kufanya maboresho kwa kuleta vifaa vya kisasa ambavyo vitakuwa sehemu salama.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete alisema wananchi wanapaswa kujipanga kwa sababu serikali imeonesha nia ya dhati ya kuboresha vituo hivyo ili wakulima waweze kunufaika.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli aliishukuru serikali kwa kuendelea kuvitambua vituo hivyo na kwamba maboresho yatakayofanyika yataleta tija kwa kuwasaidia wakulima na wafugaji. Awali akisoma taarifa, Ofisa Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Augustino Nyenza alisema kituo hicho kinakabiliwa na tatizo la uchakavu wa majengo pamoja na baadhi ya zana za kilimo kuchakaa.

Ofisa Kilimo Kata ya Lugenge, Goodlove Michael alisema kituo hicho cha Kisilo kimenufaisha wakulima 2, 294 wa kata hiyo pamoja na wakulima wa maeneo ya jirani.

Nao baadhi ya wakulima akiwemo, Frank Mwabena alisema kituo hicho kimewasaidia sana kwenye kilimo na mifugo hivyo aliomba serikali kuboresha kwa kuwapelekea zana za kisasa zinazoendana na wakati.

# Kukithiri matukio ya mauaji kwamkera RC

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amechukizwa na kukithiri kwa matukio ya mauaji, ukatili wa kijinsia ikiwemo ubakaji jambo ambalo linasababisha kuchafua taswira ya mkoa huo.

Mtaka aliyasema hayo mwisho mwa wiki wakati akizungumza kwenye kikao na makundi mbalimbali katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe chenye lengo la kutafuta mwarobaini ili jamii iweze kuondokana na matukio hayo.

Mtaka alisema matukio yanayotokea yanaondoa ubinadamu na kufedhehesha utu wa mtu na haki, hivyo jambo hilo halivumiliki.

"Kwa kweli ni matukio ambayo mimi binafsi yamenifedhehesha sana, yamenisikitisha sana, tunataka kujenga jamii ipi, huu utamaduni unatoka wapi" alisema Mtaka.

Alisema: "Nadhani serikali tumezungumza hili jambo kijuu juu siyo kwenye uzito ambao unafanana na hiki kinachotokea hizi siku za karibuni mtaona huko mitandaoni matukio kila unaposoma unajiuliza haya matukio yanafanywa na binadamu kabisa mwenye akili timamu," alisema Mtaka.

Mtaka alisema ni tofauti na mikoa mingine ambayo Kamanda wa Polisi anashughulika na mambo ya uhalifu lakini Njombe matukio mengi yanafanywa ndani ya familia.

"Sasa imekuwa kazi ya Jeshi la Polisi ni kuripoti leo kuna kituko hiki, ni matukio ambayo yapo nje ya uwezo wa kusema kwamba polisi wameshindwa kufanya kazi yao," alisema.

Alisema jamii na kila mmoja kwenye nafasi yake ya uongozi au mazingira jambo hilo linapaswa kuzungumzwa kwa uzito mkubwa.

"Hatuwezi kuwa na mkoa ambao ukiamka unaona mitandaoni mwanamke kakata mwanaume sehemu za siri sasa hapo RPC anahusikaje? mara kuna mwanaume ameingiza mkono kwenye maumbile ya nyuma ya mwanamke katoa utumbo, sasa hapo polisi anahusikaje," alihoji Mtaka.

Aidha Mtaka alisema kama tatizo ni afya ya akili basi viongozi wa dini wanapaswa kuhubiri katika nyumba zao za ibada ikiwemo makanisani na misikitini.

"Pengine viongozi wa kisiasa huko sasa tuzungumze, tujiseme, tusemane, unasoma mitandao mpaka unashangaa kwamba sisi mkoa tumepata shida gani, lakini historia ya hapa ni ya matukio ya visa mara watoto wamefanya hivi mara vile, wakati wengine huoni ushirikina unaona ushetani," alisema Mtaka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alisema kwa upande wa matukio ya mauaji kuanzia mwaka 2021 hadi Desemba mwaka 2024 matukio 279 yameripotiwa.

Alisema kwa upande wa matukio ya ukatili wa kijinsia kwa upande wa ubakaji kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2024 matukio zaidi ya 820 yameripotiwa. "Kuongezeka kwa matukio hayo ni kutokana na kuzidi kuelimisha ndivyo watu wanavyojitokeza kufika katika vituo vya polisi, lakini kitakwimu inaonesha watoto wadogo kuanzia miaka mitatu hadi 17 hawa ndio wengi ni waathirika na kwa watu wazima kuanzia miaka 18 na kuendelea matukio ni machache mno lakini katika hawa watoto umri unaoathirika zaidi ni miaka tisa mpaka miaka miwili," alisema Banga.

Alisema kwa upande wa makosa ya ulawiti kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2024 matukio 91 yameripotiwa na kwamba hilo ni tatizo lingine jipya kwa sababu wanaolawitiwa ni watoto wadogo kati ya miaka mitatu hadi miaka 17 na yanatokea ndani ya familia.

Alisema sababu ya mauaji katika wilaya za Mkoa wa Njombe, ni imani za kishirikina, migogoro ya ardhi na familia pamoja na wivu wa kimapenzi

Mmoja wa wakazi mkoani Njombe, Joram Hongoli alisema tatizo kubwa la uwepo wa matukio hayo ni kutokana na wazazi na walezi kujiondoa katika jukumu la malezi.



# Dk. Mwinyi: AAKIA utatoa huduma bora za kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema uimarishaji wa miundombinu katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume (AAKIA) kunalenga kukifanya kuwa bora na kutoa huduma kulingana na vigezo vya kimataifa.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua miradi miwili na kuweka mawe ya msingi katika miradi mitatu ya miundombinu mbalimbali katika Uwanja cha Ndege wa Kimataifa Abeid Amani Karume, Wilaya ya Magharibi B, ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema kuwa lengo ni kuwa na viwanja vya ndege vyenye sifa ya utoaji wa huduma bora kwa abiria zitakavyokidhi mahitaji ya ongezeko la wageni wanaoingia nchini kila siku.

Alisema kuwa miradi aliyoizindua itaufanya uwanja huo kuwa wa kujivunia na hadhi ya kimataifa katika Afrika na duniani kwa utoaji wa huduma bora zitakazoridhiwa na wageni.

Miradi aliyoizindua Dk. Mwinyi ni pamoja uwekaji wa mawe ya msingi kwa majengo ya abiria "Terminal 1 na 2, ambayo ameielezea itajumuisha ujenzi wa jengo la viongozi na wageni mashuhuri (VIP), utakaotumiwa pia na wafanyabiashara wakubwa, kupokea ndege binafsi za wageni mashuhuri.

Akizungumzia ukuaji wa utalii nchini alisema takribani watalii milioni mbili wanaingia nchini kila mwaka, hivyo kuna kila sababu kwa serikali kuchukua juhudi maalumu za kuimarisha viwanja vya ndege kwa miundombinu bora.

Vilevile, aliahidi ujenzi wa hoteli kubwa zenye hadhi ya juu ili kuwavutia wageni wengi zaidi, hatua itakayoimarisha utalii na kuongeza mapato yanayotokana na sekta hiyo muhimu kiuchumi.

# Matukio ya ajali barabarani yaongezeka kwa 10%

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTAKWIMU kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ahmada Hassan Suleiman amesema matukio ya ajali barabarani Zanzibar katika kipindi cha Novemba yalikuwa 21 kutoka 19 yaliyokuwa Oktoba mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.5.

Alitoa takwimu hizo juzi kwa waandishi wa habari na kusema kipindi cha Novemba 2024, Wilaya ya Magharibi A Unguja, imeripotiwa ajali nane na Wilaya ya Kaskazini A ajali nane.

Ahmada alisema ajali za barabarani kwa mwaka zimeongezeka kwa asilimia 50.0 na kufikia ajali 21 kwa Novemba 2024 kutoka ajali 14 kipindi kama hicho mwaka jana.

Alisema waathirika 54 wa ajali hizo waliripotiwa kipindi cha Novemba 2024, kati ya hao 46 walikuwa wanaume na wanane ni wanawake, huku Wilaya ya Magharibi A iliripotiwa kuwa na waathirika 22 sawa na asilimia 40.7 ikilinganishwa na wilaya zingine.

Alisema kuwa waathirika waliofariki idadi yao imeongezeka kwa asilimia 56.3 na kufikia 25 kutoka 16 kwa kipindi cha Oktoba 2024, huku majeruhi wakiongezeka kwa asilimia 50.0 na kufikia 30 kwa mwezi huo.

**Alisema kuwa waathirika waliofariki idadi yao imeongezeka kwa asilimia 56.3 na kufikia 25 kutoka 16 kwa kipindi cha Oktoba 2024, huku majeruhi wakiongezeka ...**

Alisema kuwa waathirika waliofariki Novemba mwaka huu waliongezeka ikilinganishwa na kipindi cha Novemba mwaka jana ambao walikuwa 12.

Alisema kuwa kwa kipindi cha Novemba 2024 miongoni kwa waathirika wa ajali hizo wengi wao walikuwa abiria 24 wakifuatiwa na wanaotembea kwa miguu 18 ,waendesha baskeli na pikipiki 11 na abiria mmoja.

Alisema makosa 4,687 ya barabarani yaliripotiwa kwa kipindi cha Novemba 2024 ambapo makosa 4,674 yalifanywa na wanaume na makosa13 yaliripotiwa kwa wanawake.

Hata hivyo, alisema Wilaya ya Mjini ina idadi ya makosa yaliyokuwa 864, huku Wilaya ya Micheweni ikiwa na idadi ndogo ya makosa hayo yaliyoripotiwa ambayo ni 66.

Alisema kuwa makosa makuu yaliyoripotiwa yalikuwa ni kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 1,670) yakifuatiwa kuendesha chombo cha moto bila ya leseni, bima.

Mkuu wa Disheni ya Utafiti, Ufuatiliaji na Tathimini, Sleyum Maulid Yussuf alisema kuwa mpango wao kwa sasa ni kuendelea kutoa elimu ili kupunguza makosa hayo.

Hivyo, aliwataka wadereva kuendelea kutunza sheria ili kuondoa ajali kama hizo.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Omar Hamad alisema kuwa jeshi hilo limedhamiria ikifika mwaka 2025 gari za abiria na gari nyingine kuzifungia kifaa cha kuzibiti mwendo ili kupunguza ajali.



Mwakilishi wa jimbo la Malindi, Mohamed Salumu Ahmada akiserebuka na wimbo wa Mpewa hapokonyeki ukiimbwa na msanii Neema Mwinyi (kushoto) kwenye hafla hiyo iliyofanyika kwenye Tawi la CCM Gulioni mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Mradi uhimilivu mifumo ya chakula kuwawezesha wakulima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MRATIBU wa mradi wa uhimilivu wa mifumo ya chakula Tanzania upande wa Zanzibar, Sihaba Haji Vuai, amesema mradi huo utasaidia kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji wenye tija.

Aliyasema hayo huko Cheju, Wilaya ya Kati Unguja wakati wa ziara na kamati ya uongozi ya mradi huo pamoja na wajumbe wa bodi ya zabuni ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuangalia maeneo yanayohitaji kufanyiwa ukarabati

Alisema ziara hiyo ina lengo la kuwawezesha wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Bodi ya Zabuni kuona utekelezaji halisi uliopo katika maeneo tofauti waliyotembelea sambamba na kuchukua hatua za haraka kuhakikisha ukarabati wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji.

Alisema kuwa hatua hiyo inafanyika ili kuharakisha ujenzi wake kuwasaidia wakulima na kufaidika kupitia mradi huo.

Aliyataja maeneo mengine ambayo yanayohitaji kufanyiwa ukarabati ni maabara za utafiti wa kilimo Unguja na Pemba zinazomilikiwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (ZARI), vituo vya wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji pamoja na ukarabati wa ghala za kuhifadhia mbegu.

Katika hatua nyengne, alisema kuwa mradi huo unalenga maeneo makuu matatu ambayo ni wakulima ambao watanufaika na huduma za elimu kwa wakulima, huduma za utafiti ili kupata mbegu bora na zinaostahimili ukame na maradhi pamoja na huduma za uzalishaji wa mbegu

Alisema kupitia mradi huo Serikali ya Zanzibar inakusudia kuwainua wakulima hasa katika kuwajengea miundombinu imara itakayowasaidia katika shughuli zao za kiuchumi na uzalishaji, hivyo ziara hiyo itawarahishia wajumbe walitembelea maeneo hayo kuona umuhimu wa ukarabati wa miundombinu hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wenzake, Ramadhan Salum Othman, aliwapongeza wajumbe wa kamati ya uongozi ya mradi huo kwa kufika katika maeneo yao ya kilimo na kujionea miundombinu inayohitaji kufanyiwa ukarabati kama mradi unavyoelekeza.

Katika ziara hiyo wajumbe hao walipata fursa ya kutembelea maeneo matatu yakiwemo Mwera Kichaka Mabundi, Cheju na kumalizia Bambi ambapo mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2023.

# Waziri Mkuu aipa MWAUWASA siku 55 kukamilisha ujenzi wa tangi la maji

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amemwagiza Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Neli Msuya kuhakikisha wanatumia siku 55 kutekeleza mradi wa ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji la Bujora-Kisesa mkoani hapa.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi katika ziara yake ya kukagua utekelezaji miradi ya maendeleo mkoani hapa.

Ni baada ya kukagua mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 3.5 na uwezo wa kutunza lita milioni tano na kuhudumia wananchi zaidi ya 75,000 katika maeneo ya Bujora, Kisesa na majirani zao.

Alisema ujenzi huo ambao umefikia asilimia 93, unatakiwa kukamilika mapema iwezekanavyo ili kutoa huduma ya maji ya uhakika kwa wananchi wa Kisesa.

"Kwa hatua hii, ninajua maji yatakuja Februari 2025, Mwenyezi Mungu akitujalia kuvuka nitakuja nikute maji yameanza kutoka kwa wananchi wa Bujora, Kisesa na maeneo mengine jirani," Waziri Mkuu aliagiza.

Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA, Neli Msuya, aliahidi kutekeleza mradi huo ndani ya muda kwa kuwa kwa mujibu wa mkataba, unatakiwa kuwa umekamilika kufikia Februari 15, 2025 na kuanza kutoa huduma.

Msuya alisema mradi huo ni moja ya miradi ya kimkakati ya kuboresha huduma ya maji katika maeneo ambayo yalikuwa yanakabiliwa na shida katika upatikanaji wa maji ndani ya mkoa wa Mwanza.

Alisema kuwa katika mpango wa kuboresha huduma ya upatikanaji maji jijini Mwanza, serikali imetoa Sh. bilioni 49 kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa matangi matano yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 31, likiwamo hilo la Kisesa lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni tano.

Alitaja matangi mengine kuwa yatajengwa Nyamazobe, tangi lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 10, Buhongwa lita milioni tano, Fumagaila lita milioni 10 na Usagara lita milioni moja.

Alisema katika ujenzi wa tangi hilo, mkandarasi amepewa maelekezo mahusussi ya kuanza kazi ya kulaza mabomba kutoka kwenye kituo cha Sahwa hadi kwenye tangi hilo ambako utekelezaji mradi kwa ujumla ulianza Juni 2023 na mkandarasi amelipwa Sh. bilioni 2.9.



Mratibu wa mradi wa uhimilivu wa mifumo ya chakula Tanzania upande wa Zanzibar, Sihaba Haji Vuai ,akizungumza wakati akiwa na wakulima wa Cheju mkoa wa kati Unguja wakati alipofanya ziara ya kuwakagua wakulima. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ripoti: Ubora wa huduma za mawasiliano unazidi kupaa

**Na Mwandishi Wetu**

UBORA wa huduma za mawasiliano kupitia vifaa vya mkononi nchini, uko juu ya wastani kutokana na kuenea kwa teknolojia bora zaidi, ripoti ya ukaguzi wa hivi karibuni imeonesha.

Ripoti iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari inaonesha kuwa viwango vya ubora wa maongezi, data, utumaji na upokeaji wa video mitandaoni uko juu na huduma zinapatikana bila vikwazo.

Ripoti hiyo inafuatia ukaguzi wa utoaji huduma kwenye mikoa 17, ikiwamo 12 Tanzania Bara na mitano ya Unguja na Pemba.

Ukaguzi huo unaofanywa na TCRA kila robo mwaka, umehusisha watoa huduma wote watano wenye mitandao ya mawasiliano ya simu na intaneti kupitia vifaa vya mkononi.

Ukaguzi huo unahakiki uzingatiaji masharti ya kanuni za ubora wa huduma. Ni sehemu ya majukumu ya TCRA.

Dk. Bakari alisema mwishoni mwa wiki kuwa TCRA ilipima upatikanaji huduma, ufanisi wa mitandao ubora wa maongezi na kasi ya kusafirisha data mitandaoni kwenye mikoa iliyokaguliwa.

Ukaguzi pia ulihusu upatikanaji teknolojia za mawasiliano uzao wa pili (2G), wa tatu (3G) na wa nne (4G).

Uzao wa 2G unawezesha maongezi na meseji; 3G maongezi, meseji, data, picha na video na 4G unawezesha vyote hivi pamoja na intaneti ya kasi.

Alisema ukaguzi umeonesha kuwa kwa wastani asilimia ya kufikia viwango vya ubora imeongezeka kwa pointi 1.6, kutoka asilimia 91 hadi 92.6.

"TTCL imeongeza ubora kwa pointi nane kutoka asilimia 76 Juni hadi 86 Septemba. TCRA ilikagua mitandao ya watoa huduma za simu za mkononi mikoani Arusha, Dodoma, Iringa, Mara, Morogoro, Mwanza na Njombe.

"Mikoa mingine ni Kaskazini Pemba, Kaskazini Unguja, Ruvuma, Simiyu, Singida, Kusini Pemba, Kusini Unguja, Tanga na Zanzibar Mjini Magharibi.

"Kwa ujumla, asilimia ya kuenea kwa teknolojia za mawasiliano ya simu za mkononi miongoni mwa watu imeongezeka kwa kati ya pointi moja hadi 20 kati ya Juni na Septemba 2024," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kiwango cha kuenea kijiografia imeongezeka kwa kati ya pointi moja na 10 kipindi hicho.

Alisema simu janja zilikuwa zimeenea miongoni kwa watu kwa asilimia 33.9 Septemba 2024 kutoka 31.6 Juni mwaka huu. Laini za simu zinazotumiwa na mashine kuwasiliana kati yao zimeongezeka kwa asilimia 5.5; kutoka 962,928 hadi 1,015,820 kipindi hicho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Juni mwaka huu na Umoja wa Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO), Tanzania inaongoza Afrika Mashariki kwa kiwango cha kuenea huduma za simu za mkononi kijiografia.

Ripoti hiyo inataja sababu za mafanikio hayo kuwa ni pamoja na mfumo imara wa usimamizi wa sekta, ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano na juhudi za kufikisha huduma maeneo ya pembezoni na vijijini.

## Wazee waomba kinga dhidi ya ukatili

**Na Maulid Mmbaga**

WAZEE wameshauri kuwekwe mkakati maalumu na endelevu wa kuwakinga dhidi ya vitendo vya ukatili ili kuhakikisha usalama wao katika maeneo mbalimbali nchini.

Akitoa maoni jana mkoani Dar es Salaama wakati wa mkutano wa Baraza la Ushauri la Wazee na Tume ya Mipango kuhusu kuhakiki rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Mwenyekiti wa baraza hilo, David Sendo, alisema miongoni mwa ukatili wanaofanyiwa sana wazee kwa sasa ni kunyang'anywa mali zao na wanafamilia au wengineo.

Alisema ni muhimu kuanzishwa mifumo ya kukabiliana na vitendo vya kijinsia kwa wazee na mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili pamoja na kuimarisha afua na huduma za ustawi wa jamii kwa wasiojiweza.

"Pia kuwapo afua za kukabiliana na vitendo vya ukatili wa jinsia na huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya watoto, msaada wa kisaikolojia na afya ya akili kwa waathirika wa majanga mbalimbali, nikirejea huduma zilizotolewa na maofisa ustawi kwa waathirika wa Hanang' na Kariakoo hivi karibuni.

"Kuna huduma za uimarishaji masuala ya familia na ndoa, marekebisho ya tabia kwa watoto na watu wazima wanaokinzana na sheria, lingine ni kuboresha ustawi wa wazee ili kuimarisha, kusimamia na kufuatilia utoaji huduma ya afya kwa kundi hilo katika vituo vya serikali na binafsi ili kuendana na uhitaji wao," alisema Sendo.

Pia alishauri kuwe na sheria ya wazee itakayowezesha upatikanaji na utekelezaji huduma kwao kama stahiki yao kwa mujibu wa sera, sambamba na kuimarisha upatikanaji mahitaji muhimu kwa kundi hilo kwa kuwapatia pensheni jamii ili kuboresha ustawi wao kiuchumi.

Alisisitiza kundi la wazee litambuliwe na kupatiwa bima ya afya ya bure kwa kutambua mchango wao kwa maendeleo ya kitaifa.

Alishauri wazee kushirikishwa kwenye vyombo vya uamuzi kuanzia ngazi ya vijiji, mitaa hadi mikoa pamoja na kuanzisha programu ya kuwawezesha kiuchumi kwa kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali.

"Pia tungependa kuimarishwa kwa mifumo na taasisi za ustawi wa jamijii, ikiwamo kutungwa sheria za huduma za kijamii kwa ajili ya kuimarisha uratibu na usimamizi wa huduma bora hususani kwa wazee.

"Pia kutoa kipaumbele kwa bajeti za huduma za ustawi wa jamii, kuanzishwa kwa kitengo maalumu cha ustawi kinachojitegemea kuanzia wizara, mkoa na halmashauri ili kuimarisha huduma za ustawi kwa wazee na makundi mengine," alisema Sendo.

Mjumbe wa baraza hilo, Sabu Matimbwa, alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia yahusishe wazee pia kwa sababu wengi wao wameachwa nyuma katika eneo hilo, akisema uwezeshwaji wazee kiuchumi unapaswa kuzingatiwa.

Mzee Limo alisema kanuni za bima ya afya kwa wote zitaje mzee atapataje matibabu bure, akisisitiza kwamba ni muhimu kundi hilo kwa wale wasiojiweza kabisa wakapatiwa bima ili iwawezeshe kupata matibabu bila malipo, pamoja na kuhakikisha kwamba wanapata ulinzi stahiki na kukemea vitendo vya ukatili dhidi yao.

# Wachina 17 watuhumiwa kuendesha mgodi haramu DRC

**KINSHASA, DRC**

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imesema raia 17 wa nchini China wamekamatwa kwa tuhuma za kuendesha mgodi haramu wa dhahabu, na kwamba inaendelea na msako mkali wa uchimbaji wa madini yake bila leseni.

Hayo yalibainishwa jana, ikielezwa kuwa raia hao ambao wote ni wanaume, walikamatwa baada ya ujumbe wa serikali kufanya ziara bila kutangazwa kwenye eneo la mgodi katika kijiji cha Karhembo siku ya Alhamisi.

Waziri wa Fedha wa jimbo hilo na kaimu Waziri wa Madini, Bernard Muhindo, alisema "tuliomba watuwasilishie hati za kampuni hapakuwa na hati, sifuri, hakuna cheti, hadhi, kitambulisho cha taifa, hakuna," Muhindo alisema.

Pia alibainisha kuwa takriban raia wengine 60 wa China walikuwa kwenye eneo hilo na maofisa waliwashikilia 17 ambao walionekana kuwa wasimamizi, pamoja na baadhi ya watu kutoka Congo na nchi jirani ya Burundi.

Ubalozi wa China mjini Kinshasa haukujibu mara moja ombi la Reuters la kutoa maoni. Huku Ubalozi wa Burundi ukisema bado unasubiri maelezo kutoka kwa mwakilishi wake mjini Bukavu.

Nchi hiyo ya Afrika ya kati inasema imekuwa ikijitahidi kuzuia kampuni zisizo na leseni na katika baadhi ya makundi yenye silaha kunyonya akiba yake utajiri ya cobalt, cooper, dhahabu na madini mengine.

Ushindani kuhusu shughuli za uchimbaji madini umechochea mapigano katika eneo hilo linalopakana na Rwanda.

***TRT***




Maofisa wa zimamoto wakiwa katika jitihada za uokozi katika ajali iliyotokea baada ya basi lililojaa mizigo kugongana na lori, katika barabara kuu ya kitaifa ya Fernao Dias, Brazil, jana. **PICHA: MTANDAO.**

# Nigeria yajibu shutuma za kuhatarisha usalama wa Niger

**ABUJA, Nigeria**

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Nigeria imekanusha tuhuma zilizotolewa na Niger, ambayo iliishutumu kwa kutaka kuhatarisha usalama wake, ikieleza kuwa taifa hilo liliishutumu kutumika kama msingi wa nyuma wa kuvuruga utulivu wa Niger kwa kushirikiana na baadhi ya mataifa ya kigeni na vigogo wa utawala wa zamani nchini humo.

Serikali ya Nigeria ilieleza jana kuwa ina wasiwasi sana huku ikithibitisha kwa uthabiti kwamba hakuna wanajeshi wa Ufaransa kaskazini mwa nchi wanaojiandaa kuivuruga serikali ya Niger. Ikisisitiza kuwa madai hayo hayana msingi na yanapaswa kufutiliwa mbali.

Mzozo huo ulianza mwishoni mwa wiki iliyopita wakati Waziri wa Mambo ya Nje wa Niger aliposoma taarifa kwa vyombo vya habari kwenye televisheni ya taifa; ambako aliishutumu Nigeria kwa kutaka kuhatarisha usalama wa nchi pamoja na kushiriki katika njama kwa msaada wa mataifa ya kigeni.

Pia ilielezwa kuwa mvutano huo unakuja wakati bomba, ambalo husafirisha mafuta ya Niger hadi Benin kwenye mpaka wa Nigeria, limeharibiwa mara tatu katika muda wa chini ya wiki mbili na watu wenye silaha ambao Niamey inawatuhumu kutoka Nigeria.

Shutuma pia zilikanushwa katika taarifa ya vyombo vya habari vya Nigeria, ambayo inazingatia kwamba shambulio hilo lilitekelezwa na kundi la kigaidi la Lakurawa.

Uhusiano kati ya nchi hizo mbili ulidorora kutokana na mapinduzi ya mwaka 2023, kundwa kwa AES na kutangazwa kwa kuondoka kwake kutoka ECOWAS.

***RFI***

## Papa Francis asikitishwa na ukatili Gaza

**VATICAN**

KIONGOZI wa kanisa katoliki duniani Papa Francis ameelezea masikitiko yake makubwa juu ya athari za mzozo wa Gaza na mashambulizi ya makombora yanayowalenga watoto kwenye ukanda huo.

Kwenye hotuba yake aliyotoa katika makao makuu ya kanisa katoliki duniani mjini Vatican, kiongozi huyo wa kiroho alisema kile kinachoendelea Gaza ni ukatili na siyo vita, akizungumzia mashambulizi yanayofanywa na vikosi vya Israel kwenye ukanda huo wa Wapalestina.

Papa Francis pia alizungumzia jinsi mashambulizi hayo yalivyomzuia mwakilishi wa ngazi ya juu wa kanisa katoliki kuutembelea Ukanda wa Gaza. Akisema Kadinali Pizzaballa alizuiwa kuingia ukanda wa Gaza tofauti na alivyoahidiwa.

Vita kwenye Ukanda wa Gaza vilianza Oktoba 7 mwaka jana baada ya wapiganaji wa kundi la Hamas kuishambulia Israel na kusababisha vifo vya watu 1,200.

***DW***

## Ajali ya boti yaua 38 DRC

**KINSHASA, DRC**

WATU 38 wamefariki na zaidi ya 100 bado hawajulikani walipo nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) baada ya kivuko kilichokuwa kimezidisha mzigo kupinduka katika mto Busira.

Ilielezwa jana kuwa kivuko hicho kilikuwa kimejaa watu walioukuwa wakirudi nyumbani kwa ajili ya Krismasi na kwamba kilipinduka katika mto Burisa Ijumaa usiku, kwa mujibu wa maofisa wa eneo hilo.

Pia ilielezwa kuwa katika ajali hiyo hadi kufikia jana ilithibitishwa kwamba zaidi ya watu 20 wameokolewa huku jitihada za uokozi ikiwemo kutafuta manusura zikiendelea.

Meya wa Ingende, mji wa karibu na eneo la ajali , Joseph Kingalingali alisema kivuko hicho kilikuwa kinasafiri kaskazini-mashariki mwa Congo kama sehemu ya msafara wa vyombo vingine, na abiria walikuwa hasa wafanyabiashara waliokuwa wakirudi nyumbani kwa ajili ya Krismasi.

Ilielezwa kuwa kupinduka kwa kivuko hicho kumetokea chini ya siku nne baada ya boti nyingine kupinduka kaskazini-mashariki mwa nchi, na kusababisha vifo vya watu 25.

***DW***

# Stand United yapania kurejea Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Stand United imeonesha kudhamiria kurejea Ligi Kuu, baada ya kuitwanga Cosmopolitan mabao 3-0 katika mchezo wa Ligi ya Championship, uliochezwa Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga.

Ushindi huo unaifanya timu hiyo kupanda hadi nafasi ya tatu ya msimamo, ikifikisha pointi 26, ikiwa ni moja nyuma ya Geita Gold inayoshika nafasi ya pili kwa pointi 27 na tatu nyuma ya Mtibwa Sugar ambao ni vinara wa ligi hiyo ikiwa na pointi 29.

Hata hivyo, Standa United iliyoshuka daraja msimu wa 2020/21, imecheza michezo 13, ambao ni mmoja zaidi ya timu hizo mbili zilizo juu yake, zilizoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita.

Mabao ya washindi yalifungwa na Emmanuel Manyanda, dakika ya 28 na 83, la kwanza likiwekwa wavuni dakika ya 24 na Lucas Sendama.

Mechi nyingine iliyochezwa siku hiyo, Uwanja wa Kituo cha TFF, Mnyanjani jijini Tanga, wenyeji Africa Sports walijikuta wakipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya Kwanza.

Ushindi wa Mbeya Kwanza unaifanya timu hiyo kufikisha pointi 24 na kupanda hadi nafasi ya nne ya msimamo wa ligi hiyo.

Ikumbukwe kuwa timu mbili zitakazoshuka nafasi mbili za juu mwishoni mwa msimu zitapanda moja kwa moja Ligi Kuu, huku mshindi wa tatu na wa nne wakicheza mechi za mchujo na mshindi ataisubiri timu ya Ligi Kuu kucheza nayo pia mechi ya 'play off.'

Kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Mbuni FC iliitandika Kiluvya mabao 3-1, yakitiwa kwenye kamba na Michael Mwingwa aliyefunga mawili na Advent Pius.

Poimti tatu ilizopata Mbuni zinaifanya kufikisha alama 19, ikiwa kwenye nafasi ya nane ya msimamo wa ligi hiyo, huku Kiluvya FC ikikamata mkia, ikiwa na pointi nne tu katika michezo 13 iliyocheza mpaka sasa.

# SIMBA, YANGA, AZAM U20 ZAFUZU NANE BORA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za soka za vijana za Simba, Yanga, Azam FC chini ya miaka 20, zimefuzu hatua ya nane bora kwa timu za umri huo ambazo klabu zao zipo Ligi Kuu.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), timu nane zilizofuzu zitacheza ligi moja ili kupata timu nne za juu ambazo nazo zitacheza hatua ya nusu fainali na fainali.

Timu zilizofuzu zilikuwa kwenye vikosi viwili vya timu 16 vilivyogawanywa makundi mawili, A na B kila kundi likiwa na timu nane.

Kwa mujibu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya TFF, timu nne zilizofuzu Kundi A ni Dodoma Jiji iliooongza kundi ikiwa na pointi 16, nafasi ya pili ikichukuliwa na Azam FC, iliyomaliza na pointi 13, Tabora United imeshika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 12 na Yanga imemaliza kwenye nafasi ya nne ikiwa na pointi 11.

Timu nne ambazo hazikufanikiwa katika kundi hilo ni Pamba Jiji iliyomaliza na pointi 10, Kagera Sugar pointi 10, Mashujaa FC yenye pointi nane na Singida Black Stars iliyomaliza michezo saba bila pointi yoyote ikipoteza michezo yote.

Timu zilizofunzu nane bora kutoka Kundi B, ni JKT Tanzania iliyomaliza na pointi 15, KenGold pointi 13, Simba iliyomaliza nafasi ya tatu ikiwa na pointi 12 na Fountain Gate kwenye nafasi ya nne ikiwa na pointi 11.

Ambazo hazikufanikiwa kusonga mbele ni Prisons, iliyomaliza na pointi 11, lakini tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa umeiathiri, Namungo FC iliyomaliza nafasi ya sita na pointi tisa, Coastal Union ikiwa ya sita na KMC ikimaliza ya nane na pointi zake tatu.

**DUH! KAZI KWELI...**




Kiungo wa Simba, Debora Fernandes Mavambo, katika harakati za kuucheza mpira dhidi ya winga wa Kagera Sugar, Khassim Fekha, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera juzi na kumalizika kwa Wekundu wa Msimbazi kushinda mabao 5-2. **MPIGAPICHA WETU**

# Pamba yachomoa winga Prisons

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Pamba Jiji imeendelea kujiimarisha kwa kusajili wachezaji kwa ajili ya kufanya maboresho kipindi hiki cha dirisha dogo, baada ya kupata saini ya winga wa Prisons, Zabona Mayombya.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, imeeleza kuwa wamemsajili mchezaji huyo kutokana na uwezo mkubwa alionao, na kwamba ana uwezo wa kuisaidia timu, ikikumbukwa kuwa nyota yake ilianza kuwaka akiwa jijini Mwanza.

"Amepita klabu nyingi, lakini nyota yake ilianza kung'ara akiwa Mwanza, akiichezea Alliance FC, kazunguka klabu mbalimbali na sasa amerejea nyumbani," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Mayombya anakuwa mchezaji wa tano kusajiliwa Pamba Jiji ambayo haiko katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu hiyo iliyomaliza mzunguko wa kwanza ikiwa nafasi ya 13, ikivuna pointi 12, ilipanda daraja msimu huu na ilikuwa ikitumia asilimia kubwa wachezaji ambao imetoka nao Ligi ya Championship.

Wachezaji wengine ambao imewasajili mpaka sasa ni mawinga, Hamad Majimengi, Deus Kaseke, straika Habib Kyombo na beki wa pembeni, Cherif Ibrahim kutoka Coton Sport.

Kyombo na Kaseke, walionekana dimbani, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, Desemba 16, mwaka huu, wakati timu yao ikichapwa mabao 1-0 dhidi ya KMC.

Wakati hayo yakiendelea, Klabu ya Namungo nayo imemrejesha beki wake, Emmanuel Charles, kwa ajili ya kuboresha kikosi chao.

Huyo ni mchezaji wa pili kurudishwa, baada ya Derrick Mukombozi, ambaye naye aliachwa mwanzoni mwa msimu huu. Namungo ambayo iko nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 14, imefanya usajili wa wachezaji watatu mpaka sasa, ambapo licha ya hayo waliorudishwa, imemsajili pia Najib Mussa kutoka, Singida Black Stars.

HABARIMICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE ATAKIWA NAPOLI

KLABU ya Napoli ina nia ya kumsajili beki wa kati wa Manchester United na England, Harry Maguire, huku Galatasaray pia wakifuatilia hali ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(Athletic)***

### MUABNI LULU ULAYA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 26, kuna uwezekano mkubwa wa kuondoka katika klabu hiyo Januari, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu England zikimhitaji Mfaransa huyo. ***(Florian Plettenberg)***

### NKUNKU KUONDOKA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Christopher Nkunku mwwnye umri wa miaka 27, yuko tayari kuondoka Januari baada ya kukosa muda wa kucheza, huku Paris St-Germain, Fenerbahce na Galatasaray zote zikimhitaji mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa. ***(TBR Football)***

### JAMES AIWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kuweka dau la pauni milioni 20 kumnunua mlinda mlango wa Burnley na England, James Trafford, ambaye atakuwa na umri wa miaka 22 mwezi ujao. ***(Mirror)***

### VLAHOVIC ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kushindana na Arsenal katika juhudi za kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, 24. ***(Football Insider)***

### SANE AVUTIA TIMU KIBAO

BARCELONA, Tottenham Hotspur, Manchester United na Chelsea zote zinavutiwa na winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane, 28. ***(Sport)***

### DUBRAVKA ANUKIA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Shabab inavutiwa na dili la bei iliyopunguzwa kwa mlinda lango wa Newcastle United na Slovakia, Martin Dubravka, 35. ***(I)***

### DANSO ALENGWA WOLVES

KLABU ya Wolves inaweza kulenga uhamisho wa Januari kwa mlinzi wa kati wa Austria, Kevin Danso mwenye umri wa miaka 26, ambaye Lens inaweza kutaka kumuuza. ***(L'Equipe)***

### AKLIOUCHE AITAKA BARCA

KIUNGO mshambuliaji wa Monaco na Ufaransa, Maghnes Akliouche mwenye umri wa miaka 22, amesema angependa kuichezea Barcelona katika maisha yake ya soka. ***(Sport)***

### NELSON KURUHUSIWA

WINGA wa Arsenal, Reiss Nelson ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Fulham - ataruhusiwa kuondoka kwa washikabunduki hao msimu ujao kwa kuwa kuna uwezekano mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 hatokuwa sehemu kubwa ya mipango ya Mikel Arteta katika siku zijazo. ***(Mail Plus)***

### ROBINS AMEKATAA

BOSI wa zamani wa Coventry, Mark Robins amekataa fursa ya kuzungumza na klabu nyingine ya Championship Millwall kuhusu nafasi yao ya ukocha. ***(South London Press)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND: BADO TUNA IMANI NA GUARDIOLA

●●●Ameshinda Ligi Kuu mara sita katika miaka saba, hatutasahau hilo, tunapaswa kufanya...

**MANCHESTER, England**

ERLING Haaland alijikosoa baada ya Manchester City kufungwa Jumamosi, lakini akasema wachezaji bado wanamuunga mkono kocha Pep Guardiola.

City walionekana kutokuwa na imani, mawazo na kupigana katika kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Aston Villa ambacho kilizidisha mzozo wao wa kushangaza.

Mabingwa hao mara nne mfululizo wa Ligi Kuu England wamechapwa katika mechi sita kati ya nane zilizopita za ligi na wapo pointi tisa nyuma ya vinara Liverpool ambao wamecheza michezo miwili zaidi.

Mshambuliaji nyota Haaland, akiwa bado sawa na Mohamed Salah kileleni mwa chati ya wafungaji mabao, amefunga mabao matatu pekee ya ligi tangu mwanzoni mwa Oktoba na alisema anatakiwa kuimarika ili kuisaidia timu hiyo.

"Kwanza, ninajiangalia," alisema Haaland mwenye umri wa miaka 24, akiiambia TNT Sports.

"Sijafanya mambo vizuri, sijafunga nafasi zangu. Ni lazima nifanye vizuri zaidi, sijafanya vizuri.

"Bila shaka, kujiamini kwetu si bora zaidi. Tunajua jinsi ujasiri ulivyo muhimu na unaweza kuona kwamba unaathiri kila mwanadamu. Ndivyo ilivyo, tunapaswa kuendelea na kukaa chanya ingawa ni ngumu."

Kipigo hicho kutoka kwa Aston Villa, kiliongeza shinikizo kwa kocha Guardiola, lakini Haaland alisisitiza kuwa timu iko nyuma yake.

"Alishinda Ligi Kuu mara sita katika miaka saba, kwa hiyo hatutasahau hilo," alisema Haaland.

"Atapata suluhu. Amekuwa akifanya hivyo kila mwaka. Bado tunamwamini, tunapaswa kufanya kazi kwa bidii zaidi."

## Barcelona sasa wanachapwa tu

**BARCELONA, Hispania**

HANSI Flick amesema Barcelona inahitaji mapumziko baada ya Jumamosi kufungwa na Atletico Madrid kikiwa ni kichapo cha tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Alexander Sørloth alifunga bao la ushindi dakika ya 96 kwenye Uwanja wa Olympic baada ya Rodrigo De Paul kusawazisha bao la Pedri huku Atletico wakitoka nyuma na kufanya ushindi huo uwe wa 12 mfululizo katika mashindano yote.

Kiwango cha Atletico hakikuweza kutofautisha zaidi na cha Barca, ambao sasa wameshinda mchezo mmoja tu kati ya saba za ligi kuelekea mapumziko ya msimu wa baridi nchini Hispania.

“Sasa ni mapumziko na nadhani kila mtu anahitaji mapumziko haya,” alisema Flick katika mkutano wa waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

“Baada ya mapumziko tutafanya mazoezi na tutaonesha jinsi tulivyo imara.

“Kwetu sasa, sote tumesikitishwa na kushindwa huku kwa sababu tulicheza kwa ustadi. Sasa tutasherehekea Krismas, tutaanza mazoezi Desemba 29 na kuzingatia kile tunachoweza kufanya katika nusu ijayo ya msimu.”

Barca walikuwa pointi 10 mbele ya Atletico mwanzoni mwa Novemba, lakini kichapo cha Jumamosi kiliwafanya waanguke kwa pointi tatu nyuma ya kikosi cha Diego Simeone, ambao pia wana mchezo mkononi.

Lakini Flick alihisi kiwango cha timu yake kiliboreshwa zaidi kutoka kwa jinsi walivyocheza katika wiki za hivi karibuni, wakati wamepoteza pointi dhidi ya Real Sociedad, Celta Vigo, Real Betis, Las Palmas na Leganes.

Pedri aliwapa bao la kuongoza lililostahili dhidi ya Atletico na mchanganyiko pekee wa nafasi walizokosa na mlinda mlango mahiri Jan Oblak uliwazuia.

“Ilikuwa ajabu sana jinsi tunavyocheza,” Flick aliongeza.

“Hivi ndivyo ninavyotaka kuiona timu yangu. Ninajivunia. Inaonesha pia kwamba Atletico ni timu yenye uzoefu na wanangoja tu hii na kwao inatosha.

“Nadhani mtindo wetu, jinsi tunavyotaka kucheza, ilikuwa nzuri sana. Inasikitisha sana kwamba hatuna chochote mikononi mwetu.

“Niliwaambia nathamini sana jinsi tunavyocheza, labda tunapaswa kucheza kwa akili zaidi. Tuliadhibiwa kwa makosa mawili, lazima tujifunze juu ya mambo haya, lakini hii kwangu ndiyo njia.

“Ubora tuliocheza, jinsi tulivyocheza ... nadhani kila mtu hapa chumbani anaweza kuona hii. Hii pia ni mtindo jinsi Barca wanataka kucheza, jinsi wanavyotaka kutawala, lakini mwisho ni mpira na timu kufunga mabao mengi zaidi.”

## Zubimendi atoa sababu kuikataa Liverpool

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Real Sociedad, Martin Zubimendi, amefichua sababu zilizomfanya achukue uamuzi wa kukataa mpango wa kuhamia Liverpool msimu uliopita wa majira ya joto.

Mshindi huyo wa Euro 2024, alikuwa akihitajika sana kufuatia ushindi wa Hispania baada ya msimu mzuri katila safu ya kiungo ya La Real kwenye LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Zubimendi alitajwa kuwa shabaha kuu ya uhamisho wa Liverpool kuchukua nafasi ya pengo lililoachwa kwa kuondoka kwa Fabinho.

Licha ya kuwindwa sana na kikosi cha Arne Slot, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 aliamua kusalia katika klabu yake ya utotoni, uamuzi alioufanya ili kuhakikisha kwamba angekuwa mchezaji bora wa soka baada ya muda mrefu.

“Nilikwenda likizo, na ilinishangaza,” alisema Zubimendi kuhusu nia ya Liverpool katika mahojiano na El Diario Vasco.

“Halikuwa jambo nililokuwa nimepanga. Niliitikia hali ilipotokea. Ilikuwa wakati usio na raha kwangu. Lakini nilipima faida na hasara na nikahitimisha kuwa chaguo bora zaidi lilikuwa kubaki.”

Zubimendi aliongeza: “Niliangalia maendeleo yangu binafsi, mimi ni nani, na mradi wa klabu. Nilibaki kwa sababu nilijua msimu huu ungekuwa muhimu kwangu kwenye timu, na bado nilikuwa na hatua za kuchukua. Haikuwa ngumu kiasi hicho.

“Kulikuwa na sababu nyingi za uamuzi wangu, lakini nilikuwa mbinafsi na nilifikiria juu ya kile ambacho kilikuwa bora kwangu. Na hiyo ilikuwa kubaki.”

# SAKA MAJANGA ARSENAL



**LONDON, England**

BUKAYO Saka aliondoka Uwanja wa Selhurst Park kwa magongo Jumamosi katika ushindi wa mabao 5-1 wa Arsenal dhidi ya Crystal Palace kwenye Ligi Kuu England.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, alisema “nina wasiwasi sana” na jeraha la Saka.

Winga huyo wa England alishikilia msuli wake wa paja kabla ya kutolewa nje dakika ya 25.

Arsenal walikuwa wanaongoza kwa mabao 2-1 wakati Saka akitewa na nafasi yake kuchukuliwa na Leandro Trossard.

“Tuna wasiwasi sana kuhusu jeraha la Saka,” alisema Arteta baada ya mechi.

“Alishika msuli wake wa paja na hakuweza kuendelea. Itabidi achunguzwe lakini tuna wasiwasi mkubwa.”

Saka, mshambuliaji muhimu wa Arsenal akiwa na mchango wa mabao 15 katika mechi 15 za ligi, alikosekana mapema msimu huu kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Alijiondoa kwenye kikosi cha England Oktoba kabla ya kukosa mechi mbili za Arsenal, ikiwamo kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Bournemouth.

Suala la misuli la Saka lilikuja baada ya kocha Mikel Arteta kuthibitisha Raheem Sterling - mbadala anayewezekana katika safu ya kati - alipata jeraha katika mazoezi.

HABARI MICHEZO

# FADLU AFURAHIA 5G AKIKERWA SIMBA KURUHUSU MABAO RAHISI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu David, ameonesha furaha kwa timu yake kupata ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya Kagera Sugar, akisema ni mkubwa zaidi kuupata yeye kwenye Ligi Kuu tangu aanze kuifudisha timu hiyo, lakini akichukizwa na aina ya mabao ambayo wameruhusu dakika za mwishoni.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo uliopigwa, Uwanja wa Kaitaba, Kagera, Fadlu alisema ushindi huo ulikuwa muhimu kwa kuwa ilikuwa ni mara ya kwanza kushinda hapo kwa misimu mitatu na mkubwa zaidi kwake, na timu kwa ujumla msimu huu, pia kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza kushinda idadi kubwa ya mabao, lakini umeharibiwa na kuruhusu mabao mawili ambayo hayakuwa na ulazima wowote wa kutinga wavuni.

„Ninasema ninafuraha kwa ushindi kwa wachezaji wangu kufunga mabao matano, lakini nimehuzunishwa kuruhusu mabao mawili, haikubaliki, haifurahishi, ikikuwa ni mechi ya kuondoka na ‚clean sheets',“ alisema kocha huyo.

Alisema tatizo analoliona ni kwa wachezaji ambao waliingia kipindi cha pili ambao kwa sababu timu ilikuwa imeshashinda mabao manne, badala ya kwenda kupambana, wao walicheza kama wapo mazoezini.

„Akili ya wachezaji walioingia waliona mechi imeisha kwa hiyo waliingia na kucheza kama kukamilisha dakika, waliiweka timu matatizoni muda wote,“ alisema kocha huyo.

Alisema kwa timu ambayo inasaka pointi tatu na inasaka ubingwa haiwezi kuwa inaruhusu mabao kirahisi na kizembe namna ile, huku akisema anatarajia kukaa nao na kuwaeleza jambo hilo lisijirudia tena.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Steve Mukwala, Fabrice Ngoma, Shomari Kapombe, na Jean Ahoua, yaliyoiwezesha Simba kupata ushindi huo kwa mara ya kwanza baada ya misimu mitatu, huku ikikwea juu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufikisha jumla ya pointi 34 na kuishusha Azam yenye pointi 33 iliyorudi nafasi ya pili.

Simba imecheza mechi 13, ikishinda michezo 11, sare moja na kupoteza moja, ikifunga mabao 29 na kuruhusu matano mpaka sasa, ikisalia na mechi mbili imalize mzunguko wa kwanza.

Katika hatua nyingine, mfungaji wa bao la kwanza, Kapombe, amempongeza mchezaji mwenzake Mohamed Hussein ‚Tshabalala' kwa kumpa pasi ya bao, akisema amelipa ambacho kile yeye alikifanya misimu kadhaa iliyopita alipowahi kufanya hivyo.

“Nashukuru kwa kunipa pasi, lakini analipa kwa sababu mimi nimeshawahi kumpa pasi akafunga misimu kama miwili nyuma, anakumbuka mwenyewe,“ alisema Kapombe.

## JKT Tanzania mechi 3 bila ushindi wala bao

**Na Mwandishi Wetu**

SULUHU iliyoipata Ijumaa iliyopita timu ya JKT Tanzania ikiwa ugenini Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi dhidi ya Namungo FC, imeifanya timu hiyo kucheza mechi tatu bila kufunga bao wala kupata ushindi kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mara ya mwisho JKT Tanzania kupata ushindi na kufunga bao ilikuwa ni, Novemba 29, mwaka huu, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati mkoani Manyara, ilipoifunga Fountain Gate bao 1-0, lakini baada ya hapo imetoka suluhu mechi tatu mfululizo.

Ilifanya hivyo dhidi ya Pamba Jiji, Desemba 11, mwaka huu, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam na Mashujaa FC kwenye uwanja huo huo, Desemba 15, mwaka huu, kabla ya juzi kupata tena suluhu dhidi ya Namungo.

Suluhu hiyo inaifanya timu hiyo kufikisha pointi 19 kwenye msimamo wa ligi, ikiwa kwenye nafasi ya nane, ikicheza michezo 14, ikisalia mchezo mmoja tu kumaliza mzunguko wa kwanza.

Namungo imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza ikiwa kwenye nafasi ya 12, ikikusanya pointi 14 mpaka sasa.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, amewasifu wachezaji wake kwa kupambana kuipata pointi moja, akisema lilikuwa ni lengo lao la pili kama wakikosa zote tatu.

“Niwapongeze vijana wangu, mechi kucheza ugenini si rahisi, tulikuja hapa kwa malengo mawili, tupate pointi tatu na kama tukishindwa basi moja, na tumeipata.

“Tumetengeneza nafasi mbili hatukuzitumia na tumecheza na timu bora, niipongeze Namungo wamecheza vizuri,“ alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Namungo, Juma Mgunda, alionekana kuridhika na matokeo hayo kutokana na timu aliyocheza nayo, akisema ni moja kati ya vikosi bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa.

“Matokeo nimeyapokea vizuri tu kwa sababu nimetoka suluhu na moja kati ya timu nzuri tu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

“JKT Tanzania ni timu nzuri sana, inacheza kitimu na ina wachezaji wazuri, nimeridhika na matokeo, sasa tunakwenda kujipanga na mechi za mzunguko wa pili,“ alisema Mgunda.

HUNIWEZI...



Beki wa kulia wa Yanga, Kibwana Shomari, akimthibiti winga wa Prisons, Benedict Ngassa, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam jana. Mechi hiyo ilimalizika kwa Yanga kushinda mabao 4-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Yanga yaifukuzia Simba SC kileleni

INATOKA UK. 24

hajausukumia wavuni.

Dube alifunga bao la tatu dakika moja kabla ya kwenda mapumziko likiwa ni la nne msimu huu kwenye Ligi Kuu, akifunga katika michezo miwili tu, hilo likija baada ya kufunga mabao matatu ‚hat-trick' kwenye mchezo uliopita dhidi ya Mashujaa FC.

Mabao yake manne yanamfanya awe mmoja wa wachezaji wanaoongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye timu hiyo mpaka sasa akiungana na Bacca.

Dube alimalizia kazi iliyofanywa na Aziz Ki kumpa pasi ya upendo na kuukwamisha wavuni na kuipeleka timu yake mapumziko ikiwa na mabao matatu.

Kipindi cha pili ni kama Yanga iliridhika na matokeo, au walichoka kwani hawakuonekana bora zaidi kama kipindi cha kwanza.

Prisons nao hawakuonekana tena kutafuta bao hata la kufutia machozi, badala yake walionekana kucheza pasi fupi fupi ili kupunguza idadi ya mabao, au kupoteza muda ili mechi imalizike.

Kocha wa Yanga, Sead Ramovic, alifanya mabadiliko akiwatoa Khalid Aucho, Farid, Mzize na Job, nafasi zao zikachukuliwa na Duke Abuya, Bakari Mwamnyeto, Pacome Zouzoua na Shadrack Boka.

Dakika saba kabla mechi kumalizika, Bacca alifunga kitabu cha mabao kwa Yanga, akipachika bao la nne, akiunganisha kona iliyopigwa na Pacome.

Hata hivyo, kwa picha za marejeo, ilionekana alifunga kwa kutumia mkono. Linakuwa ni bao la nne kwa beki huyo wa kati, akiungana na Dube kuwa vinara wa mabao kwa Yanga, kila mmoja akiwa na idadi hiyo ya mabao.

Ni mechi ya 15 kwa Prisons, ambayo imemaliza mzunguko wake wa kwanza ikiwa na pointi 11, kwenye nafasi ya 14 ya msimamo wa Ligi Kuu Bara.

## Old Trafford mpya kujengwa Zanzibar

INATOKA UK. 24

vikombe nchini.

Alisema, lengo ni kuongeza vipaji ili Zanzibar iwe mshindani kimataifa katika nyanja mbalimbali za michezo.

Akizungumzia kuhusu Uwanja mpya wa Maisara (Maisra Sports Complex) aliowekea jiwe la msingi, Dk. Mwinyi aliishukuru Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwa kusimamia ipasavyo maendeleo ya ujenzi huo ambao kwa kiasi kikubwa utaimarisha sekta ya hiyo nchini.

Pia, Dk. Mwinyi alisema kuwapo kwa viwanja vya mpira wa kikapu (basket ball), mpira wa wavu (volleyball), mpira wa mikono (hand ball) na mchezo wa ‚Long tennis' kutatoa mazingira bora kwa vijana kujifundisha michezo hiyo na kuzalisha vipaji zaidi.

Aidha, alifurahishwa na kuwapo kwa kituo cha mazoezi ya viungo uwanjani hapo (fitness center) pamoja na viwanja vya kufurahishia watoto (Children playground).

Michezo
Jumatatu Desemba 23, 2024
Nipashe

## Haaland: Bado tuna imani na Guardiola

UKURASA 21



PASUA!...



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akipasua katikati ya wachezaji wa Prisons, beki wa pembeni, Samson Mwaitula (kushoto) na kiungo Abdulkarim Francis Segeja, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam jana. Mechi hiyo ilimalizika kwa Yanga kushinda mabao 4-0. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAIFUKUZIA SIMBA SC KILELENI

● ● ●Bacca, Dube vinara wao wa mabao, sasa waishusha Azam FC hadi...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wamezidi kuifukuza Simba kileleni mwa msimamo, baada ya kuwachakaza Maafande wa Prisons mabao 4-0, katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

Yalikuwa ni mabao mawili ya beki wa kati, Ibrahim Hamad 'Bacca', Prince Dube na Clement Mzize yaliyotosha kuipa pointi tatu na kuipeleka moja kwa moja hadi nafasi ya pili, ikifikisha pointi 33, nyuma ya vinara Simba wenye pointi 34.

Yanga imefikisha pointi hizo sawa na Azam FC, lakini idadi ya mabao iliyofunga jana inawafanya kufikisha mabao 23 na kuwasukumiza Wanalambalamba kwenye nafasi ya tatu ambao wamecheka na nyavu mara 22.

Iliwachukua mabingwa hao dakika 12 tu kuukwamisha mpira wavuni, kazi nzuri iliyofanywa na Dube kumweka kwenye nafasi nzuri, Mzize ambaye aliutumbukiza wavuni kwa shuti la pembeni lililomwacha kipa Sebusebu Samson akiruka bila mafanikio.

Winga wa zamani wa Simba, Haruna Chanongo, aliikosesha Prisons bao la wazi dakika tatu baada ya Yanga kupata bao, alipobaki yeye na kipa, Aboutwalib Mshery aliyekuwa langoni jana, lakini alionekana kupata kigugumizi.

Chanongo alipata bahati ya mtende baada ya Dickson Job kuanguka na kuuacha mpira ukiwa hauna mwenyewe, lakini mchezaji huyo alichezacheza na mpira kabla ya Dickson Job kuwahi na kufagia hatari hiyo.

Beki wa kati wa Prisons, Nurdin Chona, alilazimika kutoka dakika ya 30 tu ya mchezo baada ya kuumia na Emmanuel Sadoki aliingia badala yake.

Yanga walikosa mabao dakika ya 33 na 37 kupitia kwa Farid Mussa na Dube, hadi dakika tatu kabla ya kwenda mapumziko, Bacca alipopachika bao la pili.

Bao hilo lilitokana na mkwaju wa faulo iliyopigwa na Stephane Aziz Ki, ambao ulikwenda kugonga mwamba wa juu na kuzagaa langoni, huku mabeki wa Prisons wakitegeana kuokoa, kabla ya mfungaji

INAENDELEA UK. 23

## Old Trafford mpya kujengwa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inatarajia kujenga uwanja mwingine mkubwa wa kisasa wenye hadhi ya kimataifa utakaotumika kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, ambapo Tanzania, Kenya na Uganda zitakuwa mwenyeji wa fainali hizo kwa mara ya kwanza.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ndiye aliyetoa kauli hiyo wakati akiweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa viwanja vipya vya michezo, Maisara (Maisara Sports Complex), Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imelenga kujenga viwanja vya kisasa vya michezo kila wilaya pamoja na akademi za michezo (Sprots Academy) kila mkoa.

"Tuna dhamira ya kweli ya kujenga uwanja wa kisasa wa AFCON utakaofanana na ule wa Old Trafford wa Manchester United ya Uingereza," alisisitiza Rais Dk. Mwinyi.

Alisema serikali pia inakusudia kufanya marekebisho makubwa ya viwanja vya Gombani Kisiwani Pemba na Uwanja wa Mao Tse Tung, Unguja lengo likiwa ni kuwa na viwanja vya kisasda vyenye hadhi vitakavyokuwa chachu ya kuwainua vijana kimichezo.

Aliongeza kuwa dhamira nyengine ya serikali ni kujenga uwanja wa soka la ufukweni (Beach soccer) kwa hadhi ya kimataifa na kujenga bwawa kubwa la kuogelea (Swimming Pool) lenye hadhi ya Olympic, (Olympic size Swimming Pool).

Alibainisha kuwa kwa muda mrefu amekuwa akisononeshwa kwa kuwapo viwanja vibovu vyenye vumbi na matope ambavyo vijana walivitumia kuchezea michezo mbalimbali ikiwamo soka, hali ambayo imepitwa na wakati, hivyo serikali imejiandaa kujenga viwanja vipya ili kutoa fursa kwa vijana kuinua vipaji vyao na ushindani kimataifa.

Alisema bado Zanzibar ina nia ya kurudi tena kuwa mwanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hivyo ujenzi wa viwanja hivyo ni itakuwa chachu na kutoa ushawishi wa kupata uanachama huo.

Dk. Mwinyi alisema kuna kila sababu kwa Zanzibar kuwa mwanachama wa CAF kwa sababu ina timu mahiri ya "Zanzibar Heroes" inayoweza kuleta ushindani na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042